# KIAMBATISHO CHA 1

***Taarifa ya Sheria ya Ulinzi wa Haki***

*Katika Sheria ya Maboresho ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 (kuidhinishwa upya kwa IDEA, 2004), Congress ilitaka Idara ya Elimu ya Marekani kuchapisha na kusambaza 'fomu za mfano', ambazo "zinaendana na mahitaji ya [Part B of the IDEA]" na "inayotoshea kupatana na matakwa" Taarifa hii ya haki za kiutaratibu imetolewa kwa majimbo.*

***KUMBUKA: Maandishi ya italiki huashiria matakwa ya Jimbo.* Maandishi ya Time Roman yasiyo ya italiki yanaashiria matakwa ya shirikisho au ya udhibiti.**

## Fursa ya kuchunguza rekodi; ushiriki wa mzazi katika mikutano.
## 34 CFR § 300.501

(a) *Fursa ya kuchunguza rekodi.* Wazazi wa mtoto mwenye ulemavu lazima wapewe, kulingana na taratibu za §§ 300.613 hadi 300.621, fursa ya kukagua na kutathmini rekodi zote za elimu kuhusiana na—

(1) Utambulisho, tathmini na uwekaji wa kielimu wa mtoto; na

(2) Utoaji wa FAPE kwa mtoto.

*(b) Ushirki wa mzazi katika mikutano.*

(1) Wazazi wa mtoto mwenye ulemavu lazima wapewe fursa ya kushiriki katika mikutano kuhusiana na—

(i) Utambulisho, tathmini na uwekaji wa kielimu wa mtoto; na

(ii) Utoaji wa FAPE kwa mtoto.

(2) Kila shirika la umma lazima litoe taarifa inayolingana na § 300.322(a)(1) na (b)(1) ili kuhakikisha kwamba wazazi wa watoto wenye ulemavu wana fursa ya kushiriki katika mikutano iliyoelezewa katika aya ya (b)(1) ya sehemu hii.

(3) Mkutano haujumuishi mazungumzo yasiyo rasmi au kutoratibiwa yanayohusisha wafanyakazi wa shirika la umma na mazungumzo kuhusu matatizo kama vile mbinu ya ufundishaji, mipango ya masomo au uratibu wa utoaji wa huduma. Mkutano pia haujumuishi shughuli ambazo wafanyakazi wa shirika la umma hujishughulisha nazo katika kuunda pendekezo au jibu la pendekezo la mzazi ambalo litajadiliwa katika mkutano wa baadaye.

*(c) Ushiriki wa mzazi katika maamuzi ya uwekaji.*

(1) Kila shirika la umma lazima lihakikishe kwamba kila mtoto mwenye ulemavu ni mwanachama wa kundi lolote linalofanya maamuzi kuhusu uwekaji wa kielimu wa mtoto wa mzazi.

(2) Katika kutelekeza matakwa ya aya ya (c)(1) ya sehemu hii, shirika la umma lazima litumie taratibu zinazoambatana na taratibu zilizoelezewa katika § 300.322(a) hadi (b)(1).

(3) Iwapo hakuna mzazi anayeweza kushiriki katika mkutano ambapo uamuzi utafanywa kuhusiana na uwekaji wa kielimu wa mtoto wao, shirika lazima litumie mbinu nyingine kuhakikisha ushiriki wao, ikiwemo simu za mtu binafsi au za mkutano au mkutano wa video.

(4) Uamuzi wa uwekaji unaweza kufanywa na kundi bila kuhusisha mzazi, ikiwa shirika la umma haliwezi kupata ushiriki wa mzazi katika uamuzi huo. Katika kisa hiki, shirika la umma lazima liwe na rekodi ya jaribio lake la kuhakikisha ushiriki wao.

## Mawasiliano Kuhusu Haki za Kiutaratibu za 34 CFR §300.504

(a) Nakala ya haki za kiutaratibu inayopatikana kwa mtoto mwenye ulemavu *au mwanafunzi mtu mzima mwenye ulemavu* lazima itolewe kwa wazazi *au mwanafunzi mtu mzima* mara moja kwa mwaka wa shule, isipokuwa kwamba nakala pia lazima itolewe kwa wazazi –

(1) Baada ya pendekezo au ombi la mzazi kwa ajili ya tathmini;

(2) Baada ya kupokea malalamiko ya kwanza ya Jimbo na baada ya kupokea ombi la kwanza la usikilizaji *wa mchakato yakinifu;*

(3) Kwa mujibu wa taratibu za nidhamu *(angalia **Taratibu wakati wa Kuadhibu Mtoto mwenye Ulemavu,** hapa chini);* na

*(4)* Kwa ombi la mzazi *au mwanafunzi mtu mzima*.

(b) Tovuti ya Intaneti. *Kitengo cha Utawala wa Shule (SAU*) kinaweza kuweka nakala ya taarifa ya haki za kiutaratibu za sasa kwenye Tovuti yake ya Intaneti ikiwa tovuti ipo.

*Vyanzo ambavyo mzazi anaweza kuwasiliana navyo kwa msaada katika kuelewa haki za mzazi kwenye Ofisi ya Mchakato Yakinifu ya Idara ya Elimu ya Maine (207-624-6644), Maine Parent Federation (1-800-870-7746), Disability Rights Center (1-800-452-1948) na Southern Maine Parent Awareness (1-800-564-9696), na KIDS LEGAL (1-866-624-7787).*

***Mzazi anaweza kuwasilisha ombi la kutatua mzozo katika Idara ya Elimu ya Maine ikiwa mzazi anaamini kwamba kitengo cha utawala wa shule (SAU) kimekiuka matakwa chini ya Kanuni za Elimu Maalum ya Maine. (Angalia Sehemu ya Utatuzi wa Mizozo hapa chini.)***

## *Ushiriki wa Mzazi*

*Kama mzazi wa mtoto ambaye anayo au anaweza kuwa na ulemavu, una haki ya kushiriki katika mikutano inayohusu uamuzi wa ustahiki wa mtoto wako, tathmini ya kwanza au tathmini mpya, uwekaji wa kielimu au utoaji wa huduma za uingiliaji wa mapema kwa mtoto wako kuanzia anapozaliwa hadi umri wa miaka 2 au utoaji wa elimu ya umma ya bila malipo inayofaa kwa mtoto wako kuanzia umri wa miaka 3 hadi miaka 20. Ikiwa wewe ni mwanafunzi mtu mzima, una haki ya kushiriki katika mikutano inayohusu uamuzi wa ustahiki wako, tathmini ya kwanza au tathmini mpya, uwekaji wa kielimu au utoaji wa elimu ya umma inayofaa ya bila malipo.*

## TAARIFA ILIYOANDIKWA

## 34 CFR §300.503

**Taarifa**

Kitengo cha Utawala wa Shule yako (SAU) lazima kikupe taarifa iliyoandikwa (kikupe taarifa fulani katika maandishi), *angalau siku 7 kabla ya tarehe ambayo kitengo cha utawala wa shule:*

**1.** Hupendekeza kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au uwekaji wa kielimu wa mtoto wako au utoaji wa *huduma za uingiliaji wa mapema wa mtoto wako kuanzia anapozaliwa hadi umri wa miaka 2 au* elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) *kwa mtoto wako kuanzia umri wa miaka 3 hadi 20;* **au**

2. Hukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au uwekaji wa kielimu wa mtoto wako au utoaji wa *huduma za uingiliaji wa mapema wa mtoto wako kuanzia anapozaliwa hadi umri wa miaka 2 au FAPE* kwa mtoto wako *kuanzia umri wa miaka 3 hadi 20*.

**Maudhui ya taarifa**

Taarifa iliyoandikwa inapaswa:

1. Kueleza hatua *kuhusu rufaa, tathmini*, *utambulisho, programu au uwekaji* ambao SAU yako inapendekeza au kukataa kuchukua;
2. Kueleza ni kwa nini SAU yako inapendekeza au kukataa kuchukua hatua;
3. Kueleza kila taratibu ya ukaguzi, tathmini, rekodi au ripoti ambayo SAU yako ilitumia katika kuamua kupendekeza au kukataa kuchukua hatua;
4. Kujumuisha taarifa kwamba una ulinzi chini ya utoaji wa haki za kiutaratibu katika Sehemu ya B ya IDEA;
5. Kukuambia jinsi unavyoweza kupata maelezo ya haki za kiutaratibu ambazo SAU yako inapendekeza au kukataa si pendekezo la kwanza la tathmini;
6. Jumuisha nyenco za kuwasiliana na wewe kwa msaada wa kuelewa *haki zako chini ya* Sehemu ya B ya IDEA, *kama vile Ofisi ya Mchakato Yakinifu ya Idara ya Elimu ya Maine (207-624-6644), Maine Parent Federation (1-800-870-7746) na Southern Maine Parent Awareness (1-800-564-9696)*
7. Eleza machaguo mengine yoyote ambayo Timu ya mpango wa elimu mahususi (IEP) ya mtoto wako, *inayojumuisha* mzazi, ilizingatia na sababu zilizofanya machaguo hayo kukataliwa;
8. Toa maelezo ya sababu nyingine za kwa nini SAU yako ilipendekeza au kukataa hatua.
9. *Jumuisha muhtasari wa maoni yaliyotolewa na wazazi, ikiwemo maelezo ya wazazi kuhusu maendeleo ya mtoto wao; na*
10. *Majina na vyeo vya kila mwanatimu.*

**Taarifa katika lugha inayoeleweka**

Taarifa inapaswa:

**1.** Kuandikwa kwa lugha inayoeleweka na umma; **na**

2. Kutolewa katika lugha yako ya asili au mbinu nyingine ya mawasiliano unayotumia, isipokuwa iwe wazi kwamba haiwezekani kufanyika hivyo.

Ikiwa lugha yako ya asili au mbinu nyingine ya mawasiliano si lugha inayoandikwa, SAU yako lazima ihakikishe kwamba:

1. Taarifa inatafsiriwa kwako kwa maneno kupitia njia nyingine katika lugha yako ya asili au mbinu nyingine ya mawasiliano;

**2.** Unaelewa maudhui ya taarifa; **na**

3. Kuna ushahidi ulioandikwa kwamba 1 na 2 zimetimizwa.

## Lugha ya Asili
## 34 CFR §300.29

Lugha ya asili, inapotumiwa na mtu ambaye ana ufahamu mdogo wa Kiingereza, inamaanisha yafuatayo, ikiwemo tafsiri ya haki za kiutaratibu:

1. Lugha inayotumiwa kwa kawaida na mtu huyo au katika kisa cha mtoto, lugha hutumiwa kwa kawaida na wazazi wa mtoto;

2. Katika mawasiliano yote ya moja kwa moja na mtoto (ikiwemo tathmini ya mtoto), lugha inayotumiwa kwa kawaida na mtoto nyumbani au katika mazingira ya mafunzo.

Kwa mtu aliye na uziwi au upofu au mtu asiye na lugha iliyoandikwa, mbinu ya mawasiliano ni ile ambayo mtu huyo hutumia kawaida (kama vile lugha ya ishara, Breli au mawasiliano ya maneno).

## Barua ya Kielektroniki
## 34 CFR §300.505

Ikiwa SAU yako itawapa wazazi chaguo la kupokea hati kupitia barua pepe *na kuchukua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha kwamba kuna haki zinazofaa za kulinda uadilifu wa mchakato*, unaweza kuchagua kupokea yafuatayo kupitia barua pepe:

1. Taarifa iliyoandikwa;

**2.** Taarifa ya haki za kiutaratibu; **~~na~~**

*3. Taarifa iliyoandikwa mapema;*

*4. IEP;*

**5.** *Ripoti za maendeleo;* **na**

6. Taarifa zinazohusiana na *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu.

## Ridhaa ya Mzazi- Ufafanuzi

## 34 CFR §300.9

**Ridhaa**

Ridhaa inamaanisha:

1. Umefahamishwa kikamilifu katika lugha yako ya asili au mbinu nyingine ya mawasiliano (kama vile lugha ya ishara, Breli au mawasiliano ya maneno) kuhusu taarifa yote kuhusiana na hatua unayotoa ridhaa.
2. Unaelewa na kukubaliana kwa maandishi na hatua hiyo na ridhaa inaeleza hatua hiyo na kuorodhesha rekodi (ikiwa zipo) zitakazotolewa na kwa nani; **na**
3. Unaelewa kwamba ridhaa ni ya hiari kwa upande wako na unaweza kuondoa ridhaa yako wakati wowote.

Kuondoa kwako kwa ridhaa hakubatilishi (kutangua) hatua iliyotokea baada ya kutoa ridhaa yako na kabla ya kuiondoa.

Iwapo mzazi atabatilisha ridhaa ya kupokea kwa huduma za elimu maalum kwa mtoto wake baada ya mtoto kupewa elimu maalum na huduma zinazohusiana hapo awali kwa maandishi, shirika la umma halitakiwi hurekebisha rekodi za elimu za mtoto ili kutoa marejeleo yoyote kwa upokeaji wa mtoto wa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa sababu ya kubatilishwa kwa ridhaa.

## Ridhaa ya Mzazi

## 34 CFR §300.300

**Ridhaa ya tathmini ya awali**

SAU yako haiwezi kutekeleza tathmini ya awali ya mtoto wako ili kubaini iwapo mtoto wako anastahiki chini ya Sehemu ya B ya IDEA kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana bila kwanza kukupa taarifa iliyoandikwa mapema ya hatua inayopendekezwa na bila kupata ridhaa yako iliyoandikwa kama ilivyoelezwa chini ya kichwa **Ridhaa ya Mzazi.**

SAU yako lazima ifanye jitihada zinazofaa za kupata ridhaa ya ufahamu ya tathmini ya awali ili kuamua iwapo mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu.

Idhini yako ya tathmini ya kwanza haimaanishi kuwa pia umetoa idhini yako kwa SAU kuanza kutoa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako. Iwapo mtoto wako amesajiliwa katika shule ya umma au unataka kumsajilisha mtoto wako katika shule ya umma na umekataa kutoa idhini au umekosa kujibu ombi la kutoa idhini kwa tathmini ya kwanza, SAU yako inaweza, lakini haihitajiki, kutaka kufanya tathmini ya kwanza wa mtoto wako kwa kutumia upatanisho wa Sheria au malalamiko ya *ombi la usikilizaji*, mkutano wa usuluhishaji, na taratibu za usikilizaji wa kesi usio na mapendeleo (isipokuwa kama unatakiwa kufanya hivyo au kukatazwa kufanya hivyo chini ya sheria ya Jimbo. SAU yako haitakiuka majukumu yake ya kupata, kutambua na kutathmini mtoto wako ikiwa haifuatii tathmini ya mtoto wako katika hali hizi, isipokuwa sheria ya Jimbo iitake iendelee na tathmini.

*Kwa ujumla, mzazi yeyote anaweza kutoa ridhaa. Katika kisa cha wazazi waliotalakiana wenye haki na makumu yanayoshirikiwa mzazi yeyote anaweza kutoa ridhaa. Hata hivyo, katika kisa ambapo mzazi mmoja anatoa ridhaa na mwingine kukataa, usimamizi wa shule una wajibu wa kuanzisha hatua kwa kutumia ridhaa iliyotolewa.*

**Sheria maalum za tathmini ya awali ya wategemezi wa Jimbo**

Ikiwa mtoto ni mtegemezi wa Jimbo na haishi na mzazi wake —
SAU haihitaji ridhaa kutoka kwa mzazi ya tathmini ya awali ili kubaini iwapo mtoto ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa:

1. Licha ya jitihada zinazofaa za kufanya hivyo, SAU haiwezi kumpata mzazi wa mtoto;
2. Haki za wazazi zimekatishwa kwa mujibu wa sheria ya Jimbo; **au**
3. Jaji ametoa haki ya kufanya maamuzi ya kielimu na ridhaa ya tathmini ya awali kwa mtu ambaye si mzazi.

Mtegemezi wa Jimbo, kama inavyotumika katika IDEA, inamaanisha mtoto ambaye, kama ilivyobainishwa na Jimbo ambamo mtoto anaishi, ni:

1. Mtoto wa kulea;
2. Anazingatiwa kuwa mtegemezi wa Jimbo chini ya sheria ya Jimbo; **au**
3. Yuko chini ya ulinzi wa shirika la umma la ustawi wa watoto.

**Ridhaa ya mzazi ya huduma**

SAU yako ni lazima ipate idhini yako iliyoandikwa kabla ya kutoa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza.
SAU ni lazima ifanye juhudi adilifu kupata idhini yako kabla ya kutoa elimu maalum na huduma husika kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza.

Iwapo hutajibu ombi la kutoa idhini yako kwa mtoto ili mtoto wako apokee elimu maalum na huduma husika kwa mara ya kwanza, au iwapo utakataa kutoa idhini kama hiyo, SAU yako inaweza kukosa kutumia ulinzi wa haki (yaani, upatanisho, malalamiko ya *Jimbo*, mkutano wa usuluhishaji, au usikilizaji wa kesi usio na mapendeleo) ili kufikia makubaliano au uamuzi kuwa elimu maalum na huduma husika zinazopendekezwa na Timu ya IEP) ya mtoto wako zinaweza kutolewa bila idhini yako.

Ikiwa unakataa kutoa ridhaa yako ya mtoto wako kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza au ikiwa hutajibu ombi la kutoa ridhaa kama hiyo na SAU haimpi mtoto wako elimu maalum na huduma zinazohusiana ambayo ilitaka ridhaa yako, SAU yako:

1. Haikiuki takwa la *kutoa huduma zinazofaa (kwa mtoto kuanzia anapozaliwa hadi afike umri wa miaka 2) au* kuhakikisha kwamba elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) inapatikana kwa mtoto wako (*mwenye umri wa miaka 3 hadi 20)* kwa kushindwa kutoa huduma hizo kwa mtoto wako; **na**
2. Haihitajiki kuwa na mkutano wa mpango wa elimu mahususi (IEP) au kutengeneza IEO kwa ajili ya mtoto wako kwa elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo ridhaa yako ilihitajika.

**Ridhaa ya mzazi ya tathmini mpya**

SAU yako lazima ipate ridhaa yako kabla ya kumtathmini upya mtoto wako, isipokuwa SAU yako ionyeshe kwamba:

1. Ilichukua hatua zinazofaa ili kupata ridhaa ya tathmini mpya ya mtoto wako; **na**
2. Hukujibu.

Iwapo utakataa kutoa idhini ya tathmini nyingine wa mtoto wako, SAU inaweza, lakini haihitajiki, kutafuta tathmini nyingine ya mtoto wako kwa kutumia upatanisho, mkutano wa usuluhishaji, na taratibu za usikilizaji wa kesi usio na mapendeleo ili kutafuta ubatilishaji wa ukataaji wako wa kutoa idhini kwa tathmini nyingine ya mtoto wako. Kulingana na tathmini za kwanza, SAU yako haikiuki wajibu wake chini ya Sehemu ya B ya IDEA iwapo inakataa kutafuta tathmini nyingine kwa namna hii.

**Hati za juhudi adilifu ili kupata ridhaa ya mzazi**

Shule yako lazima ihifadhi hati za jitihada zinazofaa ili kupata ridhaa ya mzazi ya tathmini za awali, ili kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, kwa tathmini mpya na kupata wazazi wa wategemezi wa Jimbo kwa ajili ya tathmini za awali. Hati hizo lazima zijumuishe rekodi ya majaribio ya SAU katika maeneo haya, kama vile:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au kujaribiwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za barua zilizotumwa kwa wazazi na majibu yoyote yaliyopokelewa; **na**
3. Rekodi za kina za ziara zilizofanywa kwa nyumba ya mzazi au mahali pa kazi na matokeo ya ziara hizo.

**Matakwa mengine ya ridhaa**

Ridhaa yako haihitajiki kabla ya SAU yako:

1. Kukagua data iliyopo kama sehemu ya tathmini ya mtoto wako au tathmini mpya; **au**
2. Kumpa mtoto wako mtihani au tathmini nyingine inayotolewa kwa watoto wote isipokuwa, kabla ya mtihani au tathmini, ridhaa ihitajike kutoka kwa wazazi wote wa watoto wote.

**Marekebisho ya Ridhaa ya Mzazi kuanzia tarehe 31 Desemba, 2008:**

**§300.300 Ridhaa ya mzazi.**

1. Iwapo mzazi wa mtoto atashindwa kujibu ombi la au kukataa kutoa ridhaa ya utoaji wa awali wa elimu maalum na huduma zinazohusiana, shirika la umma-

a. Huenda lisitumie taratibu katika sehemu ndogo ya E ya sehemu hii (ikiwemo taratibu za upatanishi chini ya
§ 300.506 au taratibu za mchakato yakinifu chini ya §§300.507 hadi 300.516) ili kupata makubaliano au uamuzi kwamba huduma zinaweza kutolewa kwa mtoto;
b. Halitazingatiwa kuwa linakiuka takwa la kufanya FAPE ipatikane kwa

mtoto kwa sababu ya kushindwa kumpa mtoto elimu maalum na huduma zinazohusiana ambapo mzazi anakataa au kushindwa kutoa ridhaa; na
c. Halihitajiki kuitisha mkutano wa Timu ya IEP au kutengeneza IEP chini ya §§300.320 na 300.324 kwa mtoto huyo.

2. Iwapo, wakati wowote baada ya utoaji wa awali wa elimu maalum na huduma zinazohusiana, mzazi wa mtoto anabatilisha ridhaa katika maandishi ya utoaji unaoendelea wa elimu maalum na huduma zinazohusiana, shirika la umma-

a. Huenda lisitoe elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto, lakini lazima litoe taarifa iliyoandikwa mapema kwa mujibu wa §300.503 kabla ya kusitisha utoaji wa elimu maalum na huduma zinazohusiana;
b. Huenda lisitumie taratibu katika sehemu ndogo ya E ya sehemu hii (ikiwemo taratibu za upatanishi chini ya §300.506 au taratibu za mchakato yakinifu chini ya §§300.507 hadi 300.516) ili kupata makubaliano au uamuzi kwamba huduma zinaweza kutolewa kwa mtoto;
c. Halitazingatiwa kuwa linakiuka takwa la kuhakikisha kwamba FAPE inapatikana kwa mtoto kwa sababu ya kushindwa kumpa mtoto elimu maalum ya ziada na huduma zinazohusiana; na
d. Halihitajiki kuitisha mkutano wa Timu ya IEP au kutengeneza IEP chini ya §§300.320 na 300.324 kwa mtoto kwa ajili ya kutoa elimu maalum ya ziada na huduma zinazohusiana.

## Tathmini Huru za Elimu
## 34 CFR §300.502

### Jumla

Kama ilivyoelezwa hapa chini una haki ya *kuomba* tathmini huru ya elimu (IEE) ya mtoto wako *bila gharama yoyote kwako* ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako kwamba ilipatikana na SAU yako.

Ukiomba tathmini huru ta elimu, SAU lazima ikupe taarifa kuhusu mahali ambapo unaweza kupata tathmini huru ya elimu na kuhusu kigezo cha SAU kinachotumika kwa tathmini huru za elimu.

**Fafanuzi**

Tathmini huru ya elimu inamaanisha tathmini inayotekelezwa na mtahini aliyefuzu ambaye hajaajiriwa na SAU inayowajibika katika elimu ya mtoto wako.

Gharama ya umma inamaanisha kwamba SAU inalipia gharama kamili ya tathmini au kuhakikisha kwamba tathmini inatolewa vinginevyo bila gharama yoyote kwako, kulingana na masharti ya Sehemu ya B ya IDEA, yanayoruhusu kila Jimbo kutumia Jimbo lolote, eneo husika, vyanzo vya Shirikisho na vya kibinafsi vya usaidizi vinapatikana katika Jimbo ili kukidhi matakwa ya Sehemu ya B ya Sheria.

**Haki ya mzazi ya tathmini kwa gharama ya umma**

Una haki ya tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako kupatikana na SAU yako, kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

1. Ukiomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma ikiwa hukubaliani na tathmini ya shule ya mtoto wako, SAU yako lazima, *ndani ya siku 30*, iweze: (a) Kuwasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu ili kuonyesha kwamba tathmini ya mtoto wako inafaa; au (b) Kuhakikisha kwamba tathmini huru ya elimu inatolewa kwa gharama ya umma, isipokuwa iwapo SAU itaonyesha katika usikilizaji wa kesi kwamba tathmini iliyofanywa kwa mtoto wako haikutimiza vigezo vya SAU.
2. Ikiwa SAU yako itaomba usikilizaji na uamuzi wa mwisho ni kwamba tathmini ya SAU yako inafaa, bado una haki ya tathmini huru ya elimu, lakini si kwa gharama ya umma.
3. Iwapo utaomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako, SAU inaweza kukuuliza ni kwa nini unapinga tathmini hii ya mtoto wako iliyofanywa na SAU yako. Hata hivyo, SAU yako inaweza kukosa kuhitaji ufafanuzi na haipaswi kuchelewesha kusikofaa katika kutoa tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma au katika kuwasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu ili kuomba usikilizaji wa kesi wa kutetea tathmini ya SAU ya mtoto wako.

Una haki ya kupata tathmini huru ya elimu moja pekee ya mtoto wako kwa gharama ya umma kila wakati SAU inapofanya tathmini ya mtoto wako ambayo unakataa.

**Tathmini zilizoanzishwa na mzazi**

Ukipata tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma au kushiriki na SAU tathmini ya mtoto wako uliyopata kwa gharama binafsi:

1. SAU yako lazima izingatie matokeo ya tathmini ya mtoto wako, ikiwa yatatimiza vigezo vya SAU vya tathmini huru za elimu, katika uamuzi wowote unaofanywa kwa utoaji wa elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako ; **na**
2. Wewe au SAU yako mnaweza kutoa tathmini kama ushahidi wa mchakato yakinifu kuhusiana na mtoto wako.

Maombi ya tathmini na maafisa wa usikilizaji

Ikiwa afisa wa usikilizaji anaomba tathmini huru ya elimu ya mtoto wako kama sehemu ya usikilizaji wa mchakato yakinifu, gharama ya tathmini lazima iwe kwa gharama ya umma.

**Vigezo vya SAU**

Iwapo tathmini huru ya elimu ni kwa gharama ya umma, vigezo ambavyo tathmini hii itapatikana, ikiwa ni pamoja na eneo la tathmini na sifa za mtathmini, ni lazima vifanane na vigezo ambavyo SAU inatumia inapoanzisha tathmini kwa kiwango ambacho vigezo hivi vinaendana na haki yako ya kupata tathmini huru ya elimu. Isipokuwa kwa vigezo vinavyoelezwa hapo juu, SAU haipaswi kuweka masharti au ratiba ya muda inayohusiana na upataji wa tathmini huru ya elimu kwa gharama ya umma.

# Usiri wa Maelezo

## Fafanuzi
## 34 CFR §300.611

Kama inavyotumika chini ya kichwa **Usiri wa Taarifa**:

- Uharibifu unamaanisha uharibifu halisi au uondoaji wa vitambulisho vya kibinafsi kutoka kwa maelezo ili maelezo yasiweze kutambulisha mtu binafsi.
- Rekodi za Elimu inamaanisha aina ya rekodi zinazoangaziwa katika ufafanuzi wa "rekodi za elimu" katika Sehemu ya 99 ya 34 CFR (kanuni zinazotekeleza Sheria ya Faragha na Haki za Kielimu za Familia ya 1974, 20 U.S.C. 1232g (FERPA)).
- Shirika linalohusika linamaanisha SAU yoyote, shirika, au taasisi inayokusanya, kuhifadhi au kutumia maelezo yanayoweza kutambulisha mtu binafsi au pale ambapo maelezo yanatoka, chini ya Sehemu ya B ya IDEA.

## Inayotambulisha Mtu Binafsi
## 34 CFR §300.32

Inayotambulisha mtu binafsi inamaanisha taarifa iliyo na:

(a) Jina la mtoto wako, jina lako kama mzazi au jina la mwanafamilia mwingine;
(b) Anwani ya mtoto wako;
**(c)** Kitambulisho cha mtu binafsi, kama vile nambari ya usalama wa kijamii ya mtoto wako au nambari ya mwanafunzi; **au**
(d) Orodha ya sifa binafsi au taarifa nyingine zinazoweza kufanya iwezekane kumtambua mtoto wako kwa uhakika unaofaa.

## Taarifa kwa Wazazi
## 34 CFR §300.612

Shirika la Elimu la Jimbo lazima litakupe taarifa ambayo inatosha ili kuarifu wazazi kuhusu usiri wa taarifa inayotambulisha mtu binafsi:

1. Maelezo ya kiwango ambacho taarifa inatolewa katika lugha za asili za makundi mbalimbali ya watu katika Jimbo;

2. Maelezo ya watoto ambao taarifa inayotambulisha mtu binafsi hudumishwa, aina za taarifa inayofatutwa, mbinu ambazo Jimbo inanuia kutumia katika kukusanya taarifa (ikiwemo vyanzo ambavyo taarifa hukusanywa) na matumizi yanayofanywa kuhusu taarifa;
3. Muhtasari wa sera na taratibu ambazo mashirika yanayoshiriki lazima yafuate kuhusiana na uhifadhi, ufichuaji kwa wahusika wengine, udumishaji na uharibifu wa taarifa inayomtambua mtu binafsi; **na**
4. Maelezo ya haki zote za wazazi na watoto kuhusiana na taarifa hii, ikiwemo haki chini ya Sheria ya Faragha na Haki za Kielimu za Familia (FERPA) na kanuni zake za utekelezaji katika 34 CFR Sehemu ya 99.

Kabla ya shughuli yoyote kuu ya utambulisho, eneo au tathmini (ambayo pia inajulikana kama "kupata mtoto"), taarifa lazima ichapishwe au kutangazwa katika magazeti au mitandao mingine, au zote mbili, zenye mzunguko ya kutosha kuwajulisha wazazi katika Jimbo kuhusu shughuli ya kupata, kutambua na kutathmini watoto wenye uhitaji wa elimu maalum na huduma zinazohusiana.

## Haki za Ufikiaji
## 34 CFR §300.613

Shirika linaloshiriki lazima likuruhusu ukague na kutathmini rekodi zozote za elimu kuhusiana na mtoto wako zinazokusanywa, kudumishwa au kutumika na SAU yako chini ya Sehemu ya B ya IDEA. Shirika linaloshiriki lazima lizingatie ombi lako la kukaua na kutathmini rekodi zozote za elimu kuhusu mtoto wako bila ucheleweshaji na kabla ya usikilizaji wa mchakato yakinifu usioegemea upande wowote (ikiwemo mkutano wa utatuzi au usikilizaji unaohusiana na nidhamu) na isizidi siku 45 za kalenda baada ya kutuma ombi.

Haki zako za kukagua na kutathmini rekodi za elimu zinajumuisha:
1. Haki yako ya jibu kutoka kwa shirika linaloshiriki kuhusu maombi yako yanayofaa ya ufafanuzi na ufasiri wa rekodi;
2. Haki yako ya kuomba kwamba shirika linaloshiriki kutoa nakala za rekodi ikiwa huwezi kukagua kwa ufanisi na kutathmini rekodi isipokuwa upokee nakala hizo; **na**
3. Haki yako ya kuwa na mwakilishi wako akague na kutathmini rekodi zako.

Shirika linaloshiriki linaweza kuchukulia kuwa una mamlaka ya kutathmini na kukagua rekodi zinazohusiana na mtoto wako isipokuwa iwapo umeshauriwa kuwa hauna mamlaka chini ya sheria husika ya Jimbo inayosimamia masuala kama ulezi, kutengana na talaka.

## Rekodi za Ufikiaji
## 34 CFR §300.614

Kila shirika linaloshiriki lazima lidumishe rekodi ya wahusika wanaopata ufikiaji wa rekodi za elimu zilizokusanywa, kudumishwa au kutumika chini ya Sehemu ya B ya IDEA (isipokuwa ufikiaji wa wazazi na wafanyakazi walioidhinishwa wa shirika linaloshiriki), ikiwemo jina la mhusika, tarehe ya utoaji wa ufikiaji na madhumuni ambayo mhusika anaidhinishwa kutumia rekodi.

## Rekodi kwa Zaidi ya Mtoto Mmoja

## 34 CFR §300.615

Iwapo rekodi yoyote ya elimu inajumuisha maelezo ya zaidi ya mtoto mmoja, wazazi wa watoto hao wana haki ya kuchunguza na kukagua taarifa inayohusiana na mtoto wao pekee au kujua kuhusu taarifa hiyo mahususi.

## Orodha ya Aina na Maeneo ya Taarifa

## 34 CFR §300.616

Kwa ombi, kila shirika linaloshiriki lazima likupe orodha ya aina na maeneo ya rekodi za elimu zilizokusanywa, kuhifadhiwa au kutumika na shirika.

## Ada

## 34 CFR §300.617

Kila shirika linaloshiriki linaweza kutoza ada kwa nakala za rekodi zinazotolewa kwako chini ya Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa ada hiyo haikuzuii kutumia haki yako ya kukagua na kutathmini rekodi hizo.

Shirika linaloshiriki huenda lisitoze ada ya kutafuta au kupata taarifa chini ya Sehemu ya B ya IDEA.

## Marekebisho ya Rekodi kwa Ombi la Mzazi

## 34 CFR §300.618

Iwapo unaamini kwamba taarifa katika rekodi za elimu kuhusu mtoto wako zilizokusanywa, kudumishwa au kutumika chini ya Sehemu ya B ya IDEA si sahihi, zinapotosha au kukiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, unaweza kuomba shirika linaloshiriki linalodumisha taarifa kubadilisha taarifa hiyo.

Shirika linaloshiriki lazima liamue iwapo litabadilisha taarifa kwa mujibu wa ombi lako ndani ya kipindi kinachofaa baada ya kupokea ombi lako.
Iwapo shirika linaloshiriki litakataa kubadilisha taarifa kwa mujibu wa ombi lako, linaweza kukuarifu kuhusu kukataa na kukushauri kuhusu haki ya usikilizaji wa madhumuni haya kama ilivyoelezwa chini ya kichwa **Fursa ya Usikilizaji,** *hapa chini.*

## Fursa ya Usikilizaji

## 34 CFR §300.619

Shirika linaloshiriki lazima, kwa ombi, kukupa fursa ya usikilizaji ili kupinga taarifa katika rekodi za elimu kuhusiana na mtoto wako ili kuhakikisha kwamba si sahihi, zinapotosha au vinginevyo kukiuka faragha au haki nyingine za mtoto.

## Taratibu za Usikilizaji

## 34 CFR §300.621

Usikilizaji wa kupinga taarifa katika rekodi za elimu lazima zitekelezwe kulingana na taratibu za usikilizaji chini ya Sheria ya Faragha na Haki za Kielimu za Familia (FERPA).

## Matokeo ya Usikilizaji

## 34 CFR §300.620

Iwapo, kutokana na usikilizaji wa kesi, shirika linaloshiriki linaamua kwamba taarifa hii si sahihi, zinapotosha, au vinginevyo zinakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, ni lazima ibadilishe taarifa na kukuarifu kwa maandishi.

Iwapo, kutokana na usikilizaji, shirika linaloshiriki linaamua kwamba taarifa si sahihi, zinapotosha au vinginevyo kukiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, lazima likujulishe kuhusu haki yako ya kuweka katika rekodi kwamba linadumisha kwa mtoto wako kauli inayozungumzia taarifa au utoaji wa sababu zozote ambazo hukubaliani na uamuzi wa shirika linaloshiriki .

Maelezo kama haya yaliyowekwa katika rekodi za mtoto wako yanapaswa:

**1.** Kudumishwa na shirika linaloshiriki kama sehemu ya rekodi za mtoto wako mradi tu rekodi au sehemu iliyopingwa inadumishwa na shirika linaloshiriki; **na**

2. Ikiwa shirika linaloshiriki litafichua rekodi za mtoto wako au sehemu inayopingwa kwa mhusika yeyote, ufafanuzi lazima ufichuliwe kwa mhusika huyo.

## Ridhaa ya Kufichua Taarifa Inayotambulisha Mtu Binafsi

## 34 CFR §300.622

Isipokuwa iwapo maelezo yamo katika rekodi za elimu, na ufichuzi umeidhinishwa bila idhini ya mzazi chini ya Sheria ya Faragha na Haki za Kielimu za Familia (FERPA), idhini yako ni lazima ipatikane kabla ya maelezo yanayoweza kutambulisha mtu binafsi yatolewe kwa washirika mbali na mashirika yanayoshiriki. Isipokuwa chini ya hali zilizobainidhwa hapa chini, ridhaa yako haihitajiki kabla ya taarifa inayotambulisha mtu binafsi kutolewa kwa maafisa wa mashirika yanayoshiriki kwa malengo ya kuafikia masharti ya Sehemu ya B ya IDEA.

Idhini yako, au idhini ya mtoto anayestahiki ambaye amefika *umri wa miaka 18 (au amepewa uhuru)* chini ya sheria ya Jimbo, ni lazima ipatikane kabla ya taarifa inayotambulisha mtu binafsi kutolewa kwa maafisa wa mashirika yanayohusika katika utoaji au ulipiaji wa huduma za mabadiliko.
Iwapo mtoto wako ayuko, au ataelekea, katika shule ya kibinafsi ambayo iko katika SAU sawa ambako unaishi, idhini yako ni lazima ipatikane kabla ya maelezo yanayotambulisha mtu binafsi kuhusu mtoto kutolewa kati ya maafisa katika SAU ambapo shule ya kibinafsi iko na maafisa katika SAU ambapo unaishi.

## Ulinzi
## 34 CFR §300.623

Kila shirika linaloshiriki lazima lilinde usiri wa taarifa inayomtambulisha mtu binafsi katika

hatua za ukusanyaji, uwekaji, ufichuaji na uharibifu.

Afisa mmoja katika shirika linaloshiriki ni lazima achukue jukumu la kuhakikisha usiri wa taarifa inayomtambulisha mtu binafsi.

Watu wote wanaokusanya au kutumia taarifa inayomtambulisha mtu binafsi ni lazima wapokee mafunzo au maelekezo kuhusu sera na taratibu zinazohusiana na usiri chini ya Sehemu ya B ya IDEA na Sheria ya Faragha na Haki za Kielimu za Familia (FERPA).

Kila shirika linaloshiriki ni lazima lidumishe, kwa ajili ya ukaguzi wa umma, orodha ya sasa ya majina na vyeo vya wafanyakazi hao katika shirika ambao wanaweza kufikia taarifa inayomtambulisha mtu binafsi.

## Uharibifu wa Taarifa
## 34 CFR §300.624

SAU yako lazima ikujulishe wakati taarifa inayomtambulisha mtu binafsi iliyokusanywa, kudumishwa au kutumiwa haihitajiki tena kutoa huduma za kielimu kwa mtoto wako.

Taarifa hiyo lazima iharibiwe kwa ombi lako. Hata hivyo, rekodi ya kudumu ya jina la mtoto wako, anwani na nambari ya simu, darasa lake, rekodi ya uhudhuriaji, madarasa yaliyohudhuriwa, darasa lililokamilika na mwaka wa kukamilika lazima zidumishwe bila kikomo.

# Utatuzi wa migogoro

***20-A M.R.S.A. §7202 et seq.***

## Taratibu za Malalamiko ya Jimbo

Tofauti Kati ya Usikilizaji wa Mchakato Yakinifu na Taratibu za Malalamiko ya Jimbo

Kanuni za Sehemu ya B ya IDEA ziliweka taratibu tofauti za usikilizaji wa malalamiko ya Jimbo na mchakato yakinifu. *Maine hutumia michakato ya Sehemu ya B ya utatuzi wa mizozo kwa watoto wanaohudumiwa chini ya Sehemu ya C.* Kama ilivyoelezwa hapa chini, mtu au shirika lolote linaweza kuwasilisha malalmiko ya Jimbo yanayodai ukiukaji wa matakwa ya Sehemu ya B na SAU, Shirika la Elimu la Jimbo au shirika la umma. Ni wewe tu au SAU mnaoweza kuwasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu la suala lolote kuhusiana na pendekezo au ukataaji wa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au uwekaji wa kielimu wa mtoto mwenye ulemavu au utoaji wa *huduma zinazofaa (kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka 2) au* elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) kwa mtoto *(umri wa miaka 3 hadi 20.*) Ingawa wafanyakazi wa Shirika la Elimu la Jimbo lazima watatue malalamiko ya Jimbo ndani ya muda wa kalenda ya siku 60, isipokuwa iwapo muda huo unaongezwa kwa njia inayofaa, afisa wa usikilizaji wa mchakato yakinifu usioegemea upande wowote lazima asikilize

*ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu (ikiwa halitatatuliwa katika mkutano wa utatuzi au kupitia upatanishi) na kutoa uamuzi ulioandikwa ndani ya siku 45 za kalenda baada ya kipindi cha utatuzi, kama ilivyoelezwa katika hati hii chini ya kichwa Mchakato wa Utatuzi, isipokuwa afisa wa usikilizaji atoe muda mahususi ulioongezwa kwa ombi lako au la SAU. Malalamiko ya Jimbo, utatuzi na usikilizaji wa mchakato yakinifu umeelezewa kwa kina zaidi hapa chini.

## Kupitishwa kwa Taratibu za Malalamiko ya Jimbo
## 34 CFR §300.151

### Jumla

Kila Shirika la Elimu la Jimbo lazima liwe na taratibu zilizoandikwa za:

1. Kutatua malalamiko yoyote ikiwemo malalamiko yaliyawasilishwa na shirika au mtu binafsi kutoka kwa Jimbo jingine;
2. Usambazaji mkubwa wa taratibu za malalamiko ya Jimbo kwa wazazi na watu wengine walio na maslahi, ikiwa ni pamoja na vituo vya mafunzo na taarifa kwa wazazi, mashirika ya ulinzi na utetezi, vituo vya maisha ya kujitegemea na mashirika mengine yanayofaa

### Merekebisho ya ukataaji wa huduma zinazofaa

Katika kutatua malalamiko ya Jimbo ambapo Shirika la Elimu la Jimbo limepata kushindwa kutoa huduma zinazofaa, Shirika la Kielimu la Jimbo linapaswa kushughulikia:

**1.** Kushindwa kutoa huduma zinazofaa, ikiwemo hatua ya kurekebisha inayofaa ya kushughulikia mahitaji ya mtoto; **na**

**2.** Utoaji unaofaa wa siku zijazo wa huduma kwa watoto wote wenye ulemavu.

## Taratibu za Chini za Malalamiko ya Jimbo
## 34 CFR §300.152

### Kikomo cha muda; taratibu za chini

Kila Shirika la Elimu la Jimbo lazima lijumuishe katika taratibu za malalamiko ya Jimbo kipindi cha siku 60 za kalenda baada ya kuwasilishwa kwa malalamiko kwa:

1. Fanya uchunguzi huru kwenye eneo hilo, ikiwa Shirika la Elimu ya Jimbo linaamua kwamba uchunguzi ni muhimu;
2. Mpe mlalamishi fursa ya kuwasilisha taarifa ya ziada, iwe ni kwa maneno au maandishi, kuhusu madai katika malalamiko;
3. Ipe SAU au shirika jingine la umma fursa ya kujibu malalamiko, ikiwemo, angalau: (a) kwa chaguo la shirika, pendekezo la kutatua malalamiko; **na** (b) fursa ya mzazi aliyewasilisha malalamiko na shirika kukubaliana kwa hiari kushiriki katika upatanishi;
4. Kukagua taarifa zote muhimu na kufanya uamuzi huru wa iwapo SAU au shirika jingine la umma linakiuka takwa la Sehemu ya B ya IDEA; **na**

5. Kutoa uamuzi wa maandishi kwa mlalamishi unaoshughulikia kila dai katika malalamiko na kujumuisha: (a) matokeo ya kweli na hitimisho; **na** (b) sababu za uamuzi wa mwisho wa Shirika la Elimu la Jimbo.

**Kuongezwa kwa muda; uamuzi wa mwisho; utekelezaji**

Taratibu za Shirika la Elimu la Jimbo zilizoelezwa hapo juu zinapaswa:

1. Kuruhusu kuongezwa kwa kikomo cha muda wa siku 60 za kalenda ikiwa: (a) hali za kipekee zipo kuhusiana na malalamiko fulani ya Jimbo; **or** (b) mzazi na SAU au shirika jingine la umma linalohusika likubali kwa hiari kuongeza muda wa kutatua suala hilo kupitia upatanishi au njia mbadala za utatuzi wa mizozo, ikiwa zinapatikana katika Jimbo.
2. Kujumuisha taratibu za kutekeleza kwa ufanisi uamuzi wa mwisho wa Shirika la Elimu la Jimbo, ikiwa zinahitajika, ikiwemo: (a) shughuli za usaidizi wa kiufundi; (b) mashauriano; **na** (c) hatua za marekebisho ili kufikia utiifu.

Malalamiko ya Jimbo na usikilizaji wa mchakato yakinifu

Iwapo malalamiko ya Jimbo yaliyoandikwa yatapokelewa ambayo pia ni mada ya usikilizaji wa mchakato yakinifu kama ilivyoelezwa chini ya kichwa **Kuwasilisha Ombi la Usikilizaji wa Mchakato Yakinifu,** au malalamiko ya Jimbo yana masuala mengi ambayo mojawapo au zaidi ni sehemu ya usikilizaji, Jimbo lazima liweke kando malalamiko ya Jimbo au sehemu nyingine ya malalamiko ya Jimbo ambayo yanashughulikiwa katika usikilizaji wa mchakato yakinifu hadi usikilizaji ukamilike. Suala lolote katika malalamiko ya Jimbo ambalo si sehemu ya usikilizaji wa mchakato yakinifu litatatuliwa ndani ya kipindi cha wakati na taratibu zinazoelezwa hapo juu.

Iwapo suala lililotolewa katika malalamiko ya Jimbo hapo awali liliamuliwa katika mchakato yakinifu uliohusisha baadhi ya wahusika (wewe na SAU), basi uamuzi wa usikilizaji wa mchakato yakinifu ni wa mwisho kwenye suala hilo na Shirika la Elimu la Jimbo lazima lifahamishe mlalamishi kwamba uamuzi huo ni wa lazima.

Malalamiko yanayodai kutofaulu kwa SAU au shirika jingine la umma kutekeleza uamuzi wa mchakato yakinifu lazima litatuliwe na Shirika la Elimu la Jimbo.

## Kuwasilisha Malalamiko
## 34 CFR §300.153

Shirika au mtu binafsi anaweza kuwasilisha malalamiko yaliyoandikwa ya Jimbo chini ya taratibu zilizoelezwa hapo juu.

Malalamiko ya Jimbo ni lazima yajumuishe:

1. Taarifa kwamba SAU au shirika jingine la umma limekiuka takwa la Sehemu ya B ya IDEA au kanuni zake;
2. Ukweli ambao kauli hiyo inaegemea;
3. Saini na taarifa ya mawasiliano kwa ajili ya mlalamishi; na
4. Ikiwa inadai ukiukaji kuhusu mtoto mahususi;
   (a) Jina la mtoto na anwani ya makazi ya mtoto huyo;
   (b) Jina la shule ambayo mtoto anasomea;

(c) Katika kisa cha mtoto au kijana asiye na makazi, taarifa inayopatikana ya mawasiliano ya mtoto huyo na jina la shule ambapo anasomea;

**(d)** Maelezo ya hali ya tatizo la mtoto ikiwemo ukweli unauhusiana na tatizo hilo; **na**

(e) Utatuzi uliopendekezwa wa tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwa anayelalamika kwa wakati malalamiko yanawasilishwa.

Malalamiko lazima yadai ukiukaji ambao ulifanyika kwa muda usiozidi mwaka mmoja kabla ya tarehe ambapo malalamiko yalipokelewa kama ilivyoelezwa chini ya kichwa **Upitishaji wa Taratibu za Malalamiko ya Jimbo,** *isipokuwa kama muda mrefu unakubalika kwa sababu mlalamishi anaomba huduma za kufidia kwa ajili ya ukiukaji uliotokea kwa muda usiozidi miaka miwili kabla ya tarehe ambayo malalamiko yaloyoandikwa yanapokelewa na Idara ya Elimu.* Mhusika anayewasilisha malalamiko ya Jimbo lazima atume nakala ya malalamiko kwa SAU au shirika jingine la umma linalomhudumia mtoto kwa wakati mmoja ambapo mhusika huyo anawasilisha malalamiko kwa Shirika la Elimu la Jimbo.

SEA, chini ya 34 CFR 300.537, inaweza kuamua mifumo ya utekelezaji ya Jimbo kwa mikataba ya vikao vya utatuzi na mikataba ya upatanishi.

# Taratibu za U*sikilizaji* wa Mchakato Yakinifu

## Kuwasilisha *Ombi la Usikilizaji*wa Mchakato Yakinifu 34 CFR §300.507

**Jumla**

Wewe au SAU mnaweza kuwasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu la suala lolote kuhusiana na pendekezo au ukataaji wa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au uwekaji wa kielimu wa mtoto wako au utoaji wa *huduma zinazofaa (kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka 2) au* elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) kwa mtoto *mwenye umri wa miaka 3 hadi 20*.

*Ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu lazima lidai ukiukaji uliotokea kwa muda usiozidi miaka miwili kabla ya wewe au SAU kujua au kuhitajika kujua kuhusu hatua inayodaiwa inayounda msingi wa *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu.

Muda uliotajwa hapo juu hauhusiki kwako ikiwa hukuwasilisha*ombi la usikilizaji*wa mchakato yakinifu ndani ya muda huo kwa sababu:

1. SAU ilipotosha hasa kwamba ilikuwa imetatua masuala yaliyotambulishwa katika *ombi la usikilizaji;* **au**
2. SAU ilizuia taarifa kutoka kwako kwamba ilihitajika kukupa chini ya Sehemu ya B ya IDEA.

**Taarifa kwa wazazi**

SAU lazima ikufahamishe kuhusu huduma ya bila malipo au ya bei nafuu ya kisheria na huduma nyingine husika zinazopatikana katika eneo iwapo utaomba taarifa, **au** iwapo wewe au SAU mtawasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu.

## Ombi la *Usikilizaji* wa Mchakato Yakinifu

## 34 CFR §300.508

### Jumla

Ili kuomba usikilizaji, wewe au SAU (au wakili wako au wakili wa SAU) lazima mwasilishe *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu kwa mhusika mwingine. *Ombi hilo la usikilizaji* lazima lijumuishe maudhui yote yaliyoorodheshwa hapa chini na kuwekwa kuwa ya siri.
Wewe au SAU, yeyote aliyewasilisha *ombi la usikilizaji*, lazima pia alipe Shirika la Elimu la Jimbo nakala ya *ombi la usikilizaji*. *Ombi la usikilizaji* litazingatiwa kuwa limepokelewa na muda wa udhibiti unaotumika kwa usikilizaji huo utaanza kutumika, baada ya Shirika la Elimu la Jimbo kupokea nakala ya ombi linalojumuisha taarifa inayohitajika na kupokea uthibitisho wa maandishi ambao mhusika anayepinga amepokea pia kwenye ombi.

### Maudhui ya *ombi la usikilizaji*

*Ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu linapaswa kujumuisha:

1. Jina la mtoto;
2. Anwani ya makazi ya mtoto;
3. Jina la shule ya mtoto;
4. Ikiwa mtoto huyo ni mtoto au kijana asiye na makazi, taarifa ya mawasiliano ya mtoto na jina la shule ya mtoto;
5. Maelezo ya hali ya tatizo la mtoto linalohusiana na hatua iliyopendekezwa au kukataliwa, ikiwemo ukweli unauhusiana na tatizo hilo; **na**
6. Utatuzi uliopendekezwa wa tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kupatikana kwako au SAU kwa wakati huo.

### Taarifa zinazohitajika kabla ya usikilizaji kwenye *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu

Huenda wewe au SAU msiwe na usikilizaji wa mchakato yakinifu hadi wewe au SAU (au wakili wako au wakili wa SAU), awasilishe *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu unaojumuidhs taarifa iliyoorodheshwa hapo juu.

### Utoshelevu wa *ombi la usikilizaji*

Ili *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu liendelee, lazima lizingatiwe kuwa linatosha. *Ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu litachukuliwa kuwa linatosha (kuwa limekidhi mahitaji ya maudhui yaliyotajwa hapo juu) isipokuwa iwapo mhusika anayepokea *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu (wewe au SAU) mtaarifu afisa wa usikilizaji wa kesi na mhusika mwingine katika maandishi, ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea *ombi la usikilizaji*, kuwa mhusika unayepokea anaamini kwamba malalamiko ya *ombi la usikilizaji* hayaafikii matakwa yaliyoorodheshwa hapo juu.

Ndani ya siku tano za kalenda baada ya kupokea arifa ambayo mhusika anayepokea (wewe au SAU) anazingatia kwamba *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu halitoshi, afisa wa usikilizaji lazima aamue iwapo

*ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu linakidhi matakwa yaliyotajwa hapo juu na kukujulisha wewe na SAU kwa maandishi mara moja.

**Marekebisho ya *ombi la usikilizaji***

Wewe au SAU mnaweza kufanya mabadiliko katika *ombi la usikilizaji* ikiwa tu:

**1.** Mhusika mwingine anaidhinisha mabadiliko katika maandishi na anapewa fursa ya kutatua *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu kupitia mkutano wa utatuzi, kama ilivyoelezwa hapa chini; **au**

2. Kabla ya siku tano kabla ya mchakato yakinifu, afisa wa usikilizaji anatoa ruhusa ya mabadiliko hayo.

Iwapo mhusika anayelalamika (wewe au SAU) anafanya mabadiliko kwenye*ombi la usikilizaji*wa mchakato yakinifu, muda wa mkutano wa utatuzi (ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea *ombi la usikilizaji*) na muda wa utatuzi (ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea *ombi*) anza tena katika tarehe ambayo *ombi la usikilizaji* linawasilishwa.

**Jibu la shirika la elimu la eneo lako (LEA) au SAU la ombi la usikilizaji wa mchakato yakinifu**

Iwapo SAU haijatuma taarifa iliyoandikwa mapema kwako, kama ilivyoelezwa chini. ya kichwa **Taarifa Iliyoandikwa Mapema**, kuhusu mada iliyo katika *ombi lako la usikilizaji*wa mchakato yakinifu, SAU lazima, ndani ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea *ombi la usikilizaji*wa mchakato yakinifu, kukutumia jibu linalojumuisha:

1. Ufafanuzi wa ni kwa nini SAU ilipendekeza au kukataa kuchukua hatua iliyoibuka katika *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu;

2. Maelezo ya machaguo mengine yoyote ambayo Timu ya mpango wa elimu mahususi (IEP) ya mtoto wako ilizingatia na sababu zilizofanya machaguo hayo kukataliwa;

**3.** Maelezo ya kila taratibu ya ukaguzi, tathmini, rekodi, au ripoti ambayo SAU ilitumia kama umsingi wa hatua iliyopendekezwa ua kukataliwa; **na**

4. Ufafanuzi wa sababu zingine ambazo zinahusian na hatua ya SAU iliyopendekezwa au kukataliwa.

Kutoa taarifa katika vitu 1-4 vilivotajwa hapo juu hakuzuii SAU kudai kwamba *ombi lako la usikilizaji* wa mchakato yakinifu halikutosha.

**Jibu la mhusika mwingine kuhusiana na ombi lako la usikilizaji wa mchakato yakinifu**

Isipokuwa kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ndogo kilicho hapo juu, **jibu la Shirika la elimu la eneo husika (LEA) au SAU la ombi lako la usikilizaji wa mchakato yakinifu**, mhusika anayepokea *ombi lako la usikilizaji* wa mchakato yakinifu lazima, ndani ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea *ombi*, amtumie mhusika mwingine jibu linaloshughulikia masuala katika *ombi lako la usikilizaji wa mchakato yakinifu*.

## Fomu za Modeli

## 34 CFR §300.509

Shirika la Elimu la Jimbo lazima litengeneze fomu za modeli ili kukusaidia kuwasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu na malalamiko ya Jimbo. Hata hivyo, huenda Jimbo lako au SAU isikuhitaji utumie fomu hizi za modeli. Kwa hakika, unaweza kutumia fomu hii au fomu nyingine inayofaa ya modeli, mradi tu ina taarifa inayohitajika kwa kuwasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu na malalamiko ya Jimbo.

## Upatanishi

## 34 CFR §300.506

**Jumla**

SAU lazima ifanye upatanishi upatikane ili kukuruhusu wewe na SAU kutatua mizozo inayohusiana na jambo lolote chini ya Sehemu ya B ya IDEA, ikiwemo masuala yanayotokea kabla ya kuwasilisha *ombi la usikilizaji*wa mchakato yakinifu. Kwa hivyo, upatanishi unapatikana ili kutatua mizozo chini ya Sehemu B ya IDEA iwe umewasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu au la ili kuomba usikilizaji wa mchakato yakinifu kama inavyoelezwa chini ya kichwa **Kuwasilisha Ombi la Usikilizaji wa Mchakato Yakinifu.**

**Matakwa**

Taratibu lazima zihakikishe kwamba mchakato wa upatanishi:

1. Ni wa hiari kwa upande wako na wa SAU;
2. Hautumiki kupinga au kuchelewesha haki yako katika usikilizaji wa mchakato yakinifu chini ya Sehemu ya B ya IDEA; **na**
3. Unaendeshwa na mpatanishi aliyehitimu katika mbinu za upatanishi zenye ufanisi.

SAU inaweza kutengeneza taratibu ambazo zinawapa wazazi na shule zinazochagua kutotumia mchakato wa upatanishi, fursa ya kukutana, kwa wakati na eneo linalokufaa, na mhusika asiyependezwa:

1. Ambaye yuko chini ya mkataba wa kituo kinachofaa cha utatuzi wa mizozo au kituo cha mafunzo ya mzazi na taarifa au kituo cha nyenzo cha mzazi cha jumuiya katika Jimbo; **na**
2. Ambaye angeeleza manufaa na kuhimiza matumizi ya mchakato wa upatanishi kwako.

Jimbo lazima liwe na orodha ya watu ambao ni wapatanishi waliohitimu na kufahamu sheria na kanuni zinazohusiana na utoaji wa elimu maalum na huduma zinazohusiana. Shirika la Elimu la Jimbo lazima liteue wapatanishi kinasibu, kwa mzunguko au msingi mwingine usioegemea upande wowote. Jimbo linawajibika kwa gharama ya upatanishi, ikiwemo gharama ya mikutano. Kila mkutano katika mchakato wa upatanishi lazima uratibiwe kwa wakati ufaao na ufanyike mahali panapokufaa wewe na SAU.

Iwapo wewe na SAU mtatatua mzozo kupitia mchakato wa upatanishi, pande zote mbili ni lazima ziingie katika makubaliano ya kisheria ambayo yanaanzisha utatuzi huu na kwamba:

1. Hutaja kwamba majadiliano yote yayolifanyika wakati wa mchakato wa upatanishi yatabaki kuwa siri na hayapaswi kutumika kama ushahidi katika usikilizaji wowote yakinifu au kesi ya kiraia; **and**
2. Inatiwa saini na wewe na mwakilishi wa SAU ambaye yuko na mamlaka ya kuidhinisha kwa niaba ya SAU .

Makubaliano ya upatanishi yaliyoandikwa yanaweza kutekelezwa katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka husika (mahakama ambayo ina mamlaka chini ya sheria ya Jimbo kusikia katika kusikiliza aina hii ya kesi) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani. *(Angalia Sehemu ya XVI(3)(B)(9)ya sheria hii)*
Majadiliano yanayofanyika katika mchakato wa upatanisho ni lazima yawe siri. Hayapaswi kutumika kama ushahidi katika siku zijazo katika usikilizaji wa mchakato yakinifu au kesi ya kiraia katika mahakama yoyote ya Shirikisho au ya Jimbo linalopokea usaidizi kutoka kwa Sehemu B ya IDEA.

**Kutokuwa na upendeleo kwa mpatanishi**

Mpatanishi:

1. Huenda asiwe mfanyakazi wa Shirika la Elimu la Jimbo au SAU ambayo inahusika katika elimu au utunzaji wa mtoto wako; **na**
2. Hapaswi kuwa na maslahi binafsi au ya kitaalamu inayokinzana na lengo la mpatanishi.

Mtu ambaye vinginevyo anashtahiki kama mpatanishi si mfanyakazi wa SAU au shirika la Jimbo kwa sababu analipwa na shirika au SAU ili kufanya kazi kama mpatanishi.

*Wakili anaweza kuwasilisha kitengo cha utawala katika upatanishi wakati ambapo wakili anawakilisha wazazi pekee. Wakili anayemwakilisha mzazi atampa msimamizi mkuu wa kitengo cha usimamizi wa shule na Ofisi ya Mchakato Yakinifu ya Idara ya Elimu ya Maine na angalau taarifa ya maandishi iliyoandikwa siku 7 kabla ya upatanishi kwamba atakuwa akimwakilisha mzazi katika upatanishi. Wahusika wanaweza kushauriana na mawakili kabla na baada ya kushiriki katika upatanishi.*

*Ikiwa wahusika wote wawili watakubali, lazima watie saini kwenye msamaha wa taarifa iliyoandikwa siku 7 mapema ya kuhudhuria kwa wakili wa familia katika upatanishi. Nakala ya msamaha uliotiwa saini lazima utolewe kwa Ofisi ya Mchakato Yakinifu ya Idara ya Elimu.*

*Mzazi asipochagua kushiriki katika upatanishi, mzazi huyo lazima ajulishwe na mshauri wa mchakato yakinifu kutoka Idara ya Elimu ya Maine atakayejadiliana na mzazi kuhusu manufaa ya upatanishi. Ikiwa mzazi angependa kuomba upatanishi au angependa taarifa zaidi kuhusu upatanishi, mzazi huyo anaweza kuwasiliana na Ofisi ya Mchakato Yakinifu ya Idara ya Elimu kwenye 624-6644.*

## Hali ya Uwekaji wa Mtoto *Wakati wa Kusubiri Rufaa(“Tulia”)* 34 CFR §300.518

Isipikuwa kama ilivyotolewa chini ya kichwa **TARATIBU KATIKA KUWAADHIBU WATOTO WENYE ULEMAVU,** *wakati wa kutegemea upatanishi au ombi la uchunguzi wa malalamiko ya Jimbo au* wakati *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu linatumwa kwa mhusika mwingine na wakati wa kusubiri uamuzi wa usikilizaji wa mchakato yakinifu au kesi mahakamani isiyoegemea upande wowote, mtoto wako lazima abaki katika uwekaji wake wa sasa wa kielimu isipokuwa wewe na Jimbo au SAU mkubaliane vinginevyo,

Iwapo *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu linajumuisha ombi la kuandikishwa kwa mara ya kwanza katika shule ya umma, kwa ridhaa yako, lazima awekwe katika mpango wa kawaida wa shule ya umma hadi kukamilika kwa kesi kama hizo.

Iwapo *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu linajumuisha ombi la huduma za awali chini ya Sehemu ya B ya IDEA kwa mtoto anayehama kutoka kuhudumiwa chini ya Sehemu ya C ya IDEA hadi Sehemu ya B ya IDEA na ambaye hastahiki tena kwenye huduma za Sehemu ya C kwa sababu mtoto amefikisha umri wa miaka mitatu, SAU haihitajiki kutoa huduma za Sehemu ya C ambazo mtoto amekuwa akipokea. Iwapo mtoto anapatikana kustahiki chini ya Sehemu ya B ya IDEA na unatoa ridhaa ya mtoto huyo kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, basi, anaposubiri matokeo ya kesi, SAU lazima itoe elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo hazina mabishano (zile ambazo wewe na SAU mnakubaliana nazo).

## Mchakato wa Utatuzi 34 CFR §300.510

### Mkutano wa utatuzi

Ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea *ombi la usikilizaji*wa mchakato yakinifu, na kabla ya ombi la usikilizaji wa mchakato yakinifu kuanza, SAU lazima iitishe mkutano pamoja na wewe na mwanatimu au wanatimu wa mpango wa elimu mahususi (IEP) ambao wana ujuzi maalum wa ukweli uliotambulishwa katika *ombi lako la usikilizaji* wa mchakato yakinifu. Mkutano:

1. Lazima ijumjishe mwakilishi wa SAU ambaye ana mamlaka ya kufanya uamuzi kwa niaba ya SAU; **na**
2. Huenda isijumuishe wakili wa SAU isipokuwa uandamane na wakili. Wewe na

SAU mnaamua wanatimu husika wa Timu ya IEP watakaohudhuria mkutano. Madhumuni ya mkutano huo ni kujadili *ombi la usikilizaji*wa mchakato yakinifu, na ukweli ambao ndio msingi wa *ombi la usikilizaji*, ili SAU ipate fursa ya kutatua mzozo. Mkutano wa utatuzi si wa lazima ikiwa:

1. Wewe na SAU mnakubaliana kwa maandishi kusamehe mkutano; **au**

2. Wewe na SAU mnakubaliana kutumia mchakato wa upatanishi kama ilivyoelezwa chini ya kichwa **Upatanishi.**

**Muda wa utatuzi**

Iwapo SAU haijatatua *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu kwa kiwango cha kukuridhisha ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea *ombi la usikilizaji* (katika muda wa mchakato wa utatuzi), usikilizaji wa mchakato yakinifu unaweza kutokea.

Muda wa siku 45 za kalenda za kutoa uamuzi wa mwisho unaanza baada ya kuisha kwa muda wa utatuzi wa siku 30 za kalenda, na misamaha fulani ya marekebisho kufanyika kwenye muda wa utatuzi wa siku 30 za kalenda, kama ilivyoelezwa hapa chini.

Isipokuwa pale ambapo wewe na SAU mmekubaliana kusamehe mchakato wa utatuzi au kutumia upatanishi, kukosa kwako kushiriki katika mkutano wa utatuzi utachelewesha muda wa mchakato wa utatuzi na mchakato yakinifu hadi unapokubali kushiriki katika mkutano.

Iwapo baada ya kufanya jitihada zinazofaa za kuweka kumbukumbu za jitihada hizo, SAU haiwezi kupata ushiriki katika mkutano wa utatuzi, SAU inaweza, mwishoni mwa siku 30 za kalenda, kuomba kwamba afisa wa usikilizaji apuuze *ombi lako la usikilizaji*wa mchakato yakinifu.
Kumbukumbu za jitihada kama hizo lazima zijumuishe majaribio ya SAU ya kupanga wakati na mahali uliokubaliwa na wahusika wote, kama vile:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au kujaribiwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za barua zilizotumwa kwako na majibu yoyote yaliyopokelewa;
3. Rekodi za kina za ziara zilizofanywa kwa nyumba yako au mahali pa kazi na matokeo ya ziara hizo.

Iwapo SAU itashindwa kufanya mkutano wa utatuzi ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea *ombi la usikilizaji* **wa mchakato yakinifu au** kushindwa kushiriki katika mkutano wa utatuzi, unaweza kumwomba afisa wa asitishe usikilizaji wa mchakato yakinifu wa siku 45 za kalenda kuanza.

**Marekebisho kwa muda wa utatuzi wa siku 30 za kalenda**

Iwapo wewe na SAU mtakubaliana katika maandishi kusamehe mkutano wa utatuzi, basi muda wa usikilizaji wa mchakato yakinifu wa siku 45 utaanza katika siku inayofuata.
Baada ya kuanza kwa mchakato wa mkutano wa utatuzi na kabla ya mwisho wa kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda, ikiwa wewe na SAU mnakubaliana kwa maandishi kwamba hakuna makubaliano yanayowezekana, basi kipindi cha siku 45 za kalenda cha usikilizaji wa mchakato yakinifu kinaanza siku inayofuata.
Iwapo wewe na SAU mtakubali kutumia mchakato wa upatanishi, mwishoni mwa kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda, wahusika wote wanaweza kukubaliana kwa maandishi kuendelea na upatanishi hadi uamuzi ufikiwe. Hata hivyo, iwapo wewe au SAU mtajiondoa kutoka kwa mchakato wa upatanishi, kipindi cha siku 45 za kalenda cha usikilizaji wa mchakato yakinidu kitaanza katika siku inayofuata.

**Makubaliano ya utatuzi ulioandikwa**

Ikiwa utatuzi wa mzozo unafikiwa katika mkutano wa utatuzi, wewe na SAU lazima muwe na makubaliano ya kisheria ambayo:

1. Yanatiwa saini na wewe na mwakilishi wa SAU ambaye yuko na mamlaka ya kuidhinisha kwa niaba ya SAU;
   **na**
2. Yanayoweza kutekelezwa katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka husika (mahakama ya Jimbo ambayo ina mamlaka katika kusikiliza aina hii ya kesi) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani. (Angalia Sehemu ya XVI(11)(F))

**Kipindi cha ukaguzi wa makubaliano**

Iwapo wewe na SAU mtaingia katika makubaliano kutokana na utatuzi wa mkutano, mhusika yeyote (wewe au SAU) anaweza kubatilisha makubaliano ndani ya siku 3 za kazi kuanzia wakati ambapo wewe na SAU mlitia saini kwenye makubaliano.

# Usikilizaji kuhusu*Maombi ya Usikilizaji*wa Mchakato Yakinifu

## Usikilizaji wa Mchakato Yakinifu Usio na Upendeleo

## 34 CFR §300.511

**Jumla**

Wakati wowote ambapo *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu unawasilishwa, wewe au SAU inayohusika katika mtoto lazima iwe na fursa ya usikilizaji wa mchakato yakinifu, kama ilivyoelezwa katika sehemu za **Ombi la Usikilizaji wa Mchakato Yakinifu** na **Mchakato wa Utatuzi** .

**Afisa wa usikilizaji usio na upendeleo**

Kwa kiwango cha chini, afisa wa usikilizaji:

1. Lazima asiwe mfanyakazi wa Shirika la Elimu la Jimbo au SAU ambayo inahusika katika elimu au utunzaji wa mtoto. Hata hivyo, mtu si mfanyakazi wa shirika kwa sababu yeye analipwa na shirika hilo kuhudumu kama afisa wa usikilizaji;
2. Hapaswi kuwa na maslahi binafsi au ya kitaalamu inayokinzana na lengo la afisa wa usikilizaji katika kesi;
3. Lazima awe na ujuzi na kuelewa masharti ya IDEA na kanuni za Shirikisho na Jimbo kuhusiana na IDEA na tafsiri za kisheria za IDEA katika mahakama ya Shirikisho na Jimbo; **na**
4. Lazima awe na ujuzi na uwezo wa kuendesha kesi na kufanya na kuandika uamuzi, unaoambatana na kanuni zinazofaa za kisheria.

Kila SAU lazima iweke orodha ya watu wanaohudumu kama maafisa wa usikilizaji inayojumuisha taarifa ya sifa za kila afisa wa usikilizaji.

**Mada ya usikilizaji wa mchakato yakinifu**

Mhusika (wewe au SAU) anayeomba usikilizaji wa mchakato yakinifu huenda asitoe masuala katika usikilizaji wa mchakato yakinifu ambayo hayakushughulikiwa katika *ombi la usikilizaji*, isipokuwa husika yule mwingine akubali.

**Muda wa kuomba usikilizaji**

Ni lazima wewe au SAU muombe usikilizaji usio na upendeleo wa *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu ndani ya miaka miwili baada ya tarehe ambapo wewe au SAU mlijua au kupaswa kujua suala lililoshughulikiwa katika *ombi la usikilizaji*.

**Vighairi kwenye muda**

Muda uliotajwa hapo juu hauhusiki kwako ikiwa hukuwasilisha*ombi la usikilizaji*wa mchakato yakinifu kwa sababu:

1. SAU iliwakilisha vibaya kwamba ilikuwa imetatua tatizo au suala ambalo unaibua katika *ombi lako la usikilizaji*; **au**
2. SAU ilizuia taarifa kutoka kwako kwamba ilihitajika kukupa chini ya Sehemu ya B ya IDEA.

## Haki za Usikilizaji
## 34 CFR §300.512

**Jumla**

Mhusika yeyote katika usikilizaji wa mchakato yakinifu (ikiwa ni pamoja na usikilizaji wa kesi inayohusiana na taratibu za kinidhamu) ana haki ya:

1. Kuandamana ana kushauriwa na wakili na/au watu walio na maarifa maalum au mafunzo mahususi kuhusiana na matatizo ya watoto walio na ulemavu;
2. Kutoa ushahidi na kupinga, kuchunguza kwa undani, na kuhitaji mashahidi kuhudhuria;
3. Kuzuia utoaji wa ushahidi wowote katika usikilizaji ambao haujafichuliwa kwa upande huo kwa angalau siku tano kabla ya usikilizaji;
4. Kupata rekodi ya usikilizaji iliyoandikwa, au, kwa chaguo lako, ya kielektroniki, ya neno kwa neno; **na**
5. Kupata matokeo yaliyoandikwa, au, kwa chaguo lako, ya kielektroniki.

Ufichuaji wa ziada wa taarifa

Angalau siku tano za kazi kabla ya usikilizaji wa mchakato yakinifu, wewe na SAU ni lazima mfichuliane tathmini zote ambazo zilikamilishwa kabla ya tarehe hii na mapendekezo yanayohusiana na tathmini hizi ambayo wewe au SAUmnanuia kutumia katika usikilizaji wa kesi.

Afisa wa usikilizaji wa kesi anaweza kuzuia upande wowote ambao unakosa kufuata masharti haya kutoa tathmini yoyote inayohusiana au pendekezo katika usikilizaji bila idhini ya upande mwingine.

**Haki za wazazi katika usikilizaji wa kesi**

Ni lazima uwe na haki ya:

1. Hakikisha kwamba mtoto wako anawasilisha;
2. Kufungua usikilizaji wa kesi kwa umma; **na**
3. Kuwa na rekodi ya usikilizaji, na matokeo ya ukweli na uamuzi unaotolewa kwako bila malipo yoyote.

## Maamuzi ya Usikilizaji
## 34 CFR §300.513

**Uamuzi wa afisa wa usikilizaji**

Uamuzi wa afisa wa usikilizaji kuhusu iwapo mtoto wako *(kuanzia anapozaliwa hadi umri wa miaka 2)* alipokea *huduma zinazofaa au (umri wa miaka 3 hadi 20) alipokea* elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) lazima itokane na misingi thabiti.

Katika masuala yanayodai ukiukaji wa kiutaratibu, afisa wa usikilizaji anaweza kupata kwamba mtoto wako hakupokea *huduma zinazofaa au* FAPE ikiwa kuna mapungufu ya kiutaratibu:

1. Iliingilia haki ya mtoto wako ya kupata *huduma zinazofaa au* elimu ya umma inayofaa ya bila malipo;
2. Iliingilia kwa kiasi kikubwa fursa yako ya kushiriki katika mchakato wa kufanya uamuzi kuhusiana na utoaji wa *huduma zinazofaa au* elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **au**
3. Ilisababisha kunyimwa kwa faida ya kielimu.

*Taarifa ya Uamuzi wa Mwisho*
*Kila uamuzi unaofanywa katika hitimisho ya kesi kutokana na sheria hii itakuwa katika maandishi na kujumuisha matokeo ya ukweli unaotosha kuwajulisha wahusika na mwanachama yeyote wa umma kuhusu msingi wa uamuzi huo. .*

**Kifungu cha ujenzi**

Hakuna sheria zozote zilizoelezwa hapo juu zinaweza kufafanuliwa ili kuzuia afisa wa usikilizaji kuamrisha SAU kufuata masharti katika sehemu ya ulinzi wa haki ya sheria ya shirikisho chini ya Sehemu ya B ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536).

**Ombi tofauti la usikilizaji wa mchakato yakinifu**

Hakuna chochote katika sehemu ya haki za kiutaratibu ya kanuni za Shirikisho chini ya Sehemu ya B ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536) kinachoweza kufasiriwa ili kukuzuia kujaza

*ombi tofauti la usikilizaji* wa mchakato yakinifu kuhusu suala tofauti na *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu lililojazwa tayari.

**Matokeo ya uamuzi kwa jopo la ushauri na umma**

Shirika la Elimu ya Jimbo au SAU, (yoyote iliyohusika katika usikilizaji wako) baada ya kufuta taarifa nyingine inayomtambulisha mtu binafsi, linapaswa:

1. Kutoa matokeo na maamuzi katika usikilizaji wa mchakato yakinifu au rufaa katika jopo la ushauri la elimu maalum la Jimbo; **na**
2. Hakikisha kwamba matokeo na maamuzi hayo yanapatikana kwa umma.

# Rufaa

## Mwisho wa Uamuzi; Rufaa ya

## 34 CFR §300.514

**Mwisho wa uamuzi wa usikilizaji**

Uamuzi uliofanywa katika usikilizaji wa mchakato yakinifu (ikiwemo usikilizaji unaohusiana na taratibu za kinidhamu) *lazima uwe katika maandishi na* ni wa mwisho, isipokuwa kwamba mhusika yeyote anayehusika katika usikilizaji (wewe au SAU) anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi kwa kuleta mashtaka ya kiraia, kama ilivyoelezwa hapa chini.

## Muda na Urahisi wa Usikilizaji na Ukaguzi

## 34 CFR §300.515

Shirika la Elimu la Jimbo lazima lihakikishe kwamba kwa muda usiozidi siku 45 za kalenda baada ya kipindi cha siku 30 za kalenda kwa ajili mikutano ya utatuzi **au**, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa **Marekebisho kwenye kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda,** kwa muda usiozidi siku 45 za kalenda baada ya kuisha kwa kipindi cha muda uliorekebishwa:

1. Uamuzi wa mwisho unafikiwa katika usikilizaji; **na**
2. Nakala ya uamuzi inatumwa kwa kila mhusika.

Afisa wa usikilizaji anaweza kutoa uongezaji mahususi wa muda zaidi ya siku 45 za kalenda ulioelezwa hapo juu kwa ombi la mhusika yeyote.

Kila usikilizaji lazima utekelezwe kwa wakati na eneo ambalo linafaa kwako na mtoto wako.

## Mashtaka ya Kiraia, Ikiwemo Muda ambapo Hatua Hizo Zinawasilishwa 34 CFR §300.516

**Jumla**

Mhusika yeyote (wewe au SAU) ambao haukubaliani na matokeo na uamuzi wa usikilizaji wa kesi (ikiwa ni pamoja na usikilizaji unaohusiana na taratibu za kinidhamu) ana haki ya kufungua mashataka ya kiraia kuhusiana na suala ambalo lilikuwa mada ya usikilizaji wa kesi. Hatua inaweza kuletwa katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka husika (mahakama ya Jimbo ambayo ina mamlaka katika kusikiliza aina hii ya kesi) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani bila kujali kiasi cha mzozo.

*Ikiwa mzazi ana maswali yoyote kuhusu takwa hili, lazima aelekezwe kwenye Ofisi ya Mchakato Yakinifu ya Idara ya Elimu ya Maine kwenye 624-6644.*

Kikomo cha wakati

Mhusika (wewe au SAU) anayeleta mashtaka atakuwa na siku *90 kuanzia alipopokea* uamuzi wa afisa wa usikilizaji wa kuwasilisha mashtaka ya kiraia.

### Taratibu za ziada

Katika mashtaka yoyote ya kiraia, mahakama:

A. Inapokea rekodi za kesi za kiutawala;

**B.** Husikia ushahidi wa ziada wa ombi lako au ombi la SAU; **<u>na</u>**

C. Hutegemeza uamuzi wake kwenye utiifu wa ushahidi na kutoa afueni ambayo mahakama inaamua kuwa inafaa.

### Mamlaka ya mahakama ya wilaya

Mahakama ya wilaya ya Marekani yana mamlaka ya kutoa uamuzi kuhusu mashtaka yaliyoletwa chini ya Sehemu ya B ya IDEA bila kujali kiasi cha mzozo .

### Kanuni ya ujenzi

Hakuna chochote katika Sehemu ya B ya IDEA inayozuia haki, taratibu na suluhu zinazopatikana chini ya Katiba ya Marekani, Sheria ya Wamarekani wenye Ulemavu ya 1990, Title V ya Sheria ya Urekebishaji ya 1973 (Kifungu cha 504), au sheria nyingine za shirikisho zinazolinda haki za watoto wenye ulemavu, isipokuwa kwamba kabla ya kuwasilisha mashtaka ya kiraia chini ya sheria hizi zinazohitaji msaada kwamba bado inapatikana chini ya Sehemu ya B ya IDEA, taratibu za mchakato yakinifu zilizoelezwa hapo juu zinapaswa kuwekwa kwa kiwango sawa na ambacho kingehitajika ikiwa mhusika aliwasilisha hatua chini ya Sehemu ya B ya IDEA. Hii inamaanisha kwamba unaweza kuwa na suluhu chini ya sheria nyingine zinazoingiliana na zile zinazopatikana chini ya IDEA, lakini kwa ujumla, ili kupata msaada chini ya sheria hizo, lazima kwanza utumie sukuhu zinazopatikana chini. ya IDEA (*ombi la usikilizaji*wa mchakato yakinifu, mkutano wa utatuzi na taratibu za usikilizaji wa mchakato yakinifu) kabla ya kuenda moja kwa moja mahakamani.

## Ada za Mawakili

## 34 CFR §300.517

**Jumla**

Katika mashtaka au kesi yoyote inayoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA, ukishinda mahakamani, kwa busara yake, inaweza kutoa ada adilifu kwa wakili kama sehemu ya gharama kwako.

Katika mashtaka au kesi yoyote inayoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA, mahakama inaweza, kwa busara yake, inaweza kutoa ada adilifu kwa wakili kama sehemu ya gharama kwa Shirika la Elimu la Jimbo au SAU lililoshinda, ambayo yatalipwa na wakili wako, iwapo wakili: (a) aliwasilisha *ombi la usikilizaji wa mchakato yakinifu* au kesi ya mahakama ambayo mahakama imebaini kuwa isiyo na maana, isiyofaa, au isiyo na msingi; **au** (b) aliendelea kushtaki baada ya mashtaka kuwa yasiyo na maana, yasiyofaa, au bila msingi; **au**
Katika mashtaka au kesi inayoletwa chini ya Sehemu B ya IDEA, mahakama kwa busara yake, inaweza kutoa ada adilifu kwa wakili kama sehemu ya ada ya Shirika la Elimu la Jimbo au SAU linaloshinda, ambazo utalipa wewe au wakili wako, iwapo ombi lako la usikilizaji wa kesi au kesi ya baadaye mahakamani iliwasilishwa kwa sababu isiyofaa, kama vile kunyanyasa, kusababisha uchelewaji usiofaa, au kusababisha ongezeko lisilofaa la gharama ya mashtaka au kesi.

**Utoaji wa ada**

Mahakama inaamuru ada adilifu za wakili kama ifuatavyo:

1. Ada ni lazima zihusishwe na viwango vilivyopo vya kushinda katika jamii ambapo mashtaka au kesi iliibuka kwa aina na ubora wa huduma zilizotolewa. Hakuna bonasi au uzidishaji unapaswa kutumika katika kuhesabu ada zinazoamrishwa.
2. Ada hazipaswi kuamrishwa kulipwa na gharama husika hazipaswi kurejeshwa kwa mashtaka au kesi yoyote chini ya Sehemu B ya IDEA kwa huduma zilizotolewa kabla ya ofa iliyoandikwa ya usuluhishaji imetolewa kwako iwapo:

   a. Ofa imetolewa ndani ya wakati uliopendekezwa na Sheria 68 ya Sheria za Shirikisho za Utaratibu wa Mashtaka ya Kiraia au, katika hali ya usikilizaji wa kesi au ukaguzi wa Jimbo, katika wakati wowote wa zaidi ya siku 10 za kalenda kabla ya kuanza kwa usikilizaji;

   **b.** Ofa hii haijakubaliwa ndani ya siku 10 za kalenda; **na**

   c. Mahakama au afisa msimamizi wa usikilizaji wa kesi anagundua kuwa nafuu ambayo tayari ilitolewa kwako haikufai vinavyofaa ikilinganishwa na ofa ya usuluhishaji.

   Licha ya vizuizi hivi, amri ya kulipa wakili na gharama husika zinaweza kutolewa kwako iwapo utashinda na ulikuwa na sababu halali kwa kiwango kikubwa katika kukataa ofa ya usuluhishaji.
3. Ada zinaweza kukosa kuamrishwa kulipwa kuhusiana na mkutano wowote wa Timu ya mpango wa elimu mahususi (IEP) isipokuwa iwapo mkutano utafanyika kutokana na kesi ya usimamizi au kesi ya mahakama.

   Mkutano wa utatuzi, kama ilivyofafanuliwa chini ya kichwa **Mkutano wa utatuzi**, hauzingatiwi kuwa mkutano ulioitishwa kwa sababu ya usikilizaji wa kiutawala au mashtaka ya mahakama,

na pia haizingatiwi kuwa usikilizaji wa kiutawala au mashtaka ya mahakama kwa madhumuni ya masharti ya ada hizi za mawakili.

Mahakama inapunguza, kama inavyofaa, kiasi cha ada zinazoamrishwa kulipwa wakili chini ya Sehemu ya B ya IDEA iwapo mahakama itagundua kuwa:

1. Wewe au wakili wako, wakati wa uendelezaji wa kesi au usikilizaji, mlicheleweshа bila sababu usuluhishaji wa mwisho wa mgogoro;
2. Kiasi cha ada za wakili vinginevyo kilichoidhinishwa kutolewa kinazidi kwa kiwango kikubwa kiwango cha kila saa katika jamii kwa huduma sawa za wakili aliye na ujuzi, sifa na uwezo sawa;
3. Wakati uliotumiwa na huduma zilizotolewa zilikuwa nyingi zaidi ikizingatiwa mashtaka au usikilizaji; **au**
4. Wakili anayekuwakilisha hakuipatia SAU maelezo yanayofaa katika ombi la usikilizaji wa mchakato yakinifu kama ilivyoelezwa chini ya kichwa **Ombi la Usikilizaji wa Mchakato Yakinifu**.

Hata hivyo, mahakama haipaswi kupunguza ada iwapo mahakama itagundua kwamba Jimbo au SAU lilicheleweshа bila sababu suluhisho la mwisho la kesi au usikilizaji au kulikuwa na ukiukaji wa sheria za ulinzi wa haki za Sehemu ya B ya IDEA.

# Taratibu Wakati wa Kuwaadhibu Watoto Wenye Ulemavu

## Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule

## 34 CFR §300.530

**Ubainishaji kulingana na kesi**

Wafanyakazi wa shule wanaweza kuzingatia hali zozote za kipekee kulingana na kila kesi wanapoamua iwapo ubadilishaji wa uwekaji, unaofanywa kulingana na masharti yafuatayo yanayohusiana na nidhamu, yanafaa kwa mtoto aliye na ulemavu ambaye anavunja kanuni za nidhamu za shule.

**Jumla**

Kwa kiwango kuwa pia watachukua hatua kama hii kwa watoto wasio na ulemavu, wafanyakazi wa shule wanaweza, kwa **siku za shule zisizozidi 10** kwa mfululizo, kuondoa mtoto aliye na ulemavu anayekiuka kanuni za nidhamu katika uwekaji wake wa sasa kwa mazingira mbadala yanayofaa ya muda ya kielimu (ambayo lazima yaamuliwe na Timu ya mpango wa elimu mahususi (IEP) wa mtoto), mazingira mengine, au kufukuzwa. Wafanyakazi wa shule pia wanaweza kuweka uondoaji zaidi kwa mtoto wa **siku zisizozidi 10 za shule** kwa mfululizo katika mwaka uleule wa shule katika matukio tofauti ya ukosaji nidhamu, almradi uondoaji huu haujumuishi ubadilishaji wa uwekaji (angalia **Ubadilishaji wa Uwekaji kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu** kwa ajili ya ufafanuzi, hapa chini).

Pindi tu mtoto aliye na ulemavu anapoondolewa katika uwekaji wake wa sasa kwa jumla ya **siku 10 za shule** katika mwaka sawa wa shule, SAU ni lazima, wakati wa siku zinazofuata za uondoaji katika mwaka huo wa elimu shuleni, itoe huduma kwa kiwango kinachohitajika chini ya kichwa ndogo **Huduma**.

**Mamlaka ya ziada**

Iwapo tabia inayokiuka kanuni za nidhamu ya wanafunzi haikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto, (angalia **Uamuzi wa udhihirisho**, hapa chini) na ubadilishaji wa uwekaji utazidi **siku 10 za shule** kwa mfululizo, wafanyakazi wa shule wanaweza kutumia taratibu za nidhamu kwa mtoto huyu aliye na ulemavu kwa namna sawa na kwa kipindi sawa kama ingekuwa kwa watoto wasio na ulemavu, isipokuwa shule inapaswa kutoa huduma kwa mtoto huyo kama ilivyoelezwa hapo chini katika **Huduma**. Timu ya IEP ya mtoto huamua mpangilio mbadala wa mazingiwa ya elimu kwa huduma hizo.

**Huduma**

Huduma ambazo zinapaswa kutolewa kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye ametolewa kutoka kwa uwekaji wa sasa zinaweza kutolewa katika mazingira mbadala ya elimu ya muda. SAU inahitajika tu kutoa huduma kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye ametolewa kutoka kwenye uwekaji wake wa sasa kwa **siku 10 au chache za shule** katika mwaka huo wa shule, ikitoa huduma kwa mtoto asiye na ulemavu ambaye ametolewa vilevle.

Mtoto mwenye ulemavu ambaye ametolewa kutoka kwenye uwekaji wake wa sasa kwa **zaidi ya siku 10 za shule** anapaswa:

1. Aendelee kupokea huduma za kielimu, ili iwezeshe mtoto aendelee kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, hata ingawa katika mazingira mengine , na kuendelea katika kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto; **na**
2. Apokee, kama inavyotakikana, tathmini ya tabia inayoendelea, na huduma za uingiliaji wa tabia na urekebishaji, ambazo zimeundwa kushughulikia ukiukwaji wa tabia ili usifanyike tena.

Baada ya mtoto aliye na ulemavu kuondolewa katika uwekaji wake wa sasa kwa **siku 10 za shule** katika mwaka huohuo wa shule, na **iwapo** uondoaji huu wa sasa ni wa **siku 10 za shule** mfululizo au chache **na** iwapo uondoaji sio ubadilishaji wa uwekaji (angalia ufafanuzi hapo chini),**kisha** mfanyakazi wa shule, kwa kushauriana na angalau mwalimu mmoja wa mtoto, atabaini kiwango ambacho huduma zinahitajika ili kuwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine, na kuendelea katika kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto. Iwapo uondoaji ni ubadilishaji wa uwekaji (angalia ufafanuzi hapa chini), Timu ya IEP ya mtoto inabaini huduma inayofaa ili kuwezesha mtoto aendelee kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, hata ingawa katika mazingira mengine, na kuendelea katika kufikia malengo yaliyopangwa katika IEP ya mtoto.

**Ubainishaji wa udhihirishaji**

Ndani ya **siku 10 za shule** za uamuzi wowote wa kubadilisha uwekaji wa mtoto aliye na ulemavu kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni za nidhamu ya wanafunzi (isipokuwa katika uondoaji ambao ni wa **siku 10 za shule** mfululizo au chini na sio ubadilishaji wa uwekaji) SAU, mzazi na wanatimu husika

ya Timu ya IEP (kama ilivyobainishwa na mzazi na SAU) wanapaswa kukagua maelezo yoyote yanayofaa katika faili la mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na IEP ya mtoto, uchunguzi wowote wa mwalimu, na maelezo yoyote yanayofaa ya wazazi ili kubaini:

**1.** Iwapo tabia iliyokiukwa ilisababishwa na, au ilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja au kwa kiwango kikubwa na, ulemavu wa mtoto; **au**

2. Iwapo tabia iliyokiukwa ilisababishwa moja kwa moja na kushindwa kwa SAU kutekeleza IEP ya mtoto.

Iwapo SAU, mzazi na washirika wanaofaa wa Timu ya IEP ya mtoto watabaini kuwa mojawapo ya hali hizi imeafikiwa, tabia hii ni lazima ibainishwe kuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto.

Iwapo SAU, mzazi na washirika wanaofaa wa Timu ya IEP ya mtoto watabaini kuwa tabia iliyokiukwa ilisababishwa moja kwa moja na SAU kushindwa kutekeleza IEP, SAU ni lazima ichukue hatua ya moja kwa moja kusuluhisha upungufu huu.

**Ubainishaji kuwa tabia ilikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto**

Iwapo SAU, mzazi na washirika wanaofaa wa wanatimu wa IEP mtabaini kuwa tabia ilikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto, Timu ya IEP ni lazima:

**1.** Ifanye tathmini ya tabia ya kiutendaji, isipokuwa iwapo SAU ilifanya tathmini ya tabia ya kiutendaji kabla ya kufanyika kwa tabia iliyosababisha ubadilishaji wa uwekaji, na kutekeleza mpango wa uingiliaji wa tabia kwa mtoto; **au**

2. Iwapo mpango wa uingiliaji wa tabia tayari umeundwa, ifanye ukaguzi wa mpango wa uingiliaji wa tabia, na irekebishe, kama inavyohitajika, ili kutatua tabia hii.

Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapo chini ya kichwa ndogo**Hali Maalum**, SAU inapaswa irudishe mtoto katika uwekaji ambao mtoto aliondolewa, isipokuwa iwapo mzazi na wilaya mkubaliane ubadilishaji wa uwekaji kama sehemu ya urekebishaji wa mpango wa uingiliaji wa tabia.

**Hali maalum**

Iwe au isiwe kwamba tabia ilikuwa udhihirishaji wa ulemavu wa mtoto, wafanyakazi wa shule wanaweza kumwondoa mwanafunzi kwa mazingira mbadala ya elimu (iliyoamuliwa na Timu ya IEP ya mtoto) kwa siku za shule zisizozidi 45, iwapo mtoto:

1. Anaenda na silaha (angalia ufafanuzi hapo chini) shuleni au yuko na silaha akiwa shuleni, au majengo ya shule, au katika shughuli ya shule iliyo chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu la Jimbo au SAU;

**2.** Anajua anazo au anatumia dawa za kulevya (angalia ufafanuzi hapo chini), au anauza au anaomba kuuziwa bidhaa iliyodhibitiwa, (angalia ufafanuzi hapo chini), akiwa shuleni, katika majengo ya shule, au katika shughuli ya shule iliyo chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu la Jimbo au SAU; **au**

3. Amesababisha jeraha baya la mwilini (angalia ufafanuzi hapo chini) kwa mtu mwingine akiwa shuleni, au majengo ya shule, au katika shughuli ya shuleni iliyo chini ya mamlaka ya Shirika la Elimu la Jimbo au SAU.

   Fafanuzi

**Bidhaa iliyodhibitiwa** inamaanisha dawa au bidhaa nyingine iliyotambuliwa katika ratiba za I, II, III, IV, au V katika Sehemu ya 202(c) ya Sheria ya Bidhaa Zilizodhibitiwa (21 U.S.C. 812(c)).

**Dawa haramu** inamaanisha bidhaa iliyodhibitiwa, lakini haijumuishi bidhaa iliyodhibitiwa ambayo sio haramu kuimiliki au kutumika chini ya uangalizi wa mtaalamu wa huduma za kiafya aliyeidhinishwa au ambayo inamilikiwa kisheria au inatumika chini ya mamlaka nyingine yoyote chini ya Sheria hiyo au chini ya utoaji mwingine wa sheria ya Shirikisho.

**Jeraha kubwa la mwili** lina maana kwa istilahi "jeraha kubwa la mwili" chini ya aya *(3)* ya kifungu kidogo (h) cha sehemu ya 1365 ya kichwa cha 18, Kanuni ya Marekani: *Jeraha la mwili linalohusisha hatari ya kifo; maumivu makali ya kimwili; uharibifu wa muda mrefu na dhahiri au kuharibika kwa kazi ya kiungo cha mwili au akili.*

**Silaha** ina maana inayotolewa kwa neno silaha hatari chini ya aya ya (2) ya kifungu cha kwanza (g) ya sehemu ya 930 ya kichwa cha 18, Kanuni za Marekani: *Silaha, kifaa, chombo, nyenzo au kitu, kilichohuishwa au kisichohuishwa, kinachotumika kwa au kinachoweza kusababisha kifo au jeraha kubwa la mwili, isipokuwa kwamba neno kama hilo halijumuishi kisu cha mfukoni chenye ubapa wenye urefu wa inchi 2 ½.*

**Arifa**
Katika tarehe ambapo itafanya maamuzi ya kufanya uondoaji ambao ni ubadilishaji wa uwekaji wa mtoto kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni za maadili ya wanafunzi, SAU ni lazima iwaarifu wazazi kuhusu uamuzi huu, na kuwapa wazazi taarifa ya haki za kiutaratibu.

## Ubadilishaji wa Uwekaji kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu 34 CFR §300.536

Uondoaji wa mtoto mwenye ulemavu kutoka kwa uwekaji wa sasa wa kielimu ni **ubadilishaji wa uwekaji** iwapo:

1. Uondoaji huu ni wa siku zaidi ya 10 kwa mfululizo; **au**
2. Mtoto amepata mfululizo wa uondoaji ambao umekuwa ni mtindo kwa sababu:
   a. Jumla ya msururu wa uondoaji ni zaidi ya siku 10 za shule katika mwaka wa shule;
   b. Tabia ya mtoto inafanana kwa kiasi kikubwa na tabia ya mtoto katika matukio ya hapo awali ambayo yalisababisha msururu wa uondoaji;
   c. Kwa sababu kama hizi za ziada kama vile urefu wa muda wa kila uondoaji, jumla ya wakati mtoto ameondolewa, na ukaribu wa uondoaji kutoka kwa mwingine; **na**

Iwe mtindo wa uondoaji unajumuisha ubadilishaji wa uwekaji unaamuliwa kulingana na kesi na SAU na, iwapo utapingwa, unapaswa kukaguliwa kupitia mchakato wa usikilizaji wa kesi na kesi ya mahakama.

## Uamuzi wa Mazingira

## 34 CFR § 300.531

Timu ya mpango wa elimu mahususi (IEP) lazima iamue mazingira mbadala ya elimu ya muda kwa uondoaji ambayo ni **mabadiliko ya uwekaji**, na uondoaji chini ya vichwa **Mamlaka ya ziada** na **Hali maalum**, hapo juu.

## Ukataji Rufaa

## 34 CFR § 300.532

### Jumla

Mzazi wa mtoto mwenye ulemavu anaweza kuwasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu (angalia hapo juu) ili kuomba kusikilizwa kwa mchakato yakinifu ikiwa hakubaliani na:

1. Uamuzi wowote unaohusiana na uwekaji uliofanyika chini ya utoaji huu wa nidhamu; **au**
2. Ubainishaji wa udhihirishaji kama ilivyoelezwa hapo juu.

SAU inaweza kuwasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu (angalia hapo juu) ili kuomba usikilizaji wa mchakato yakinifu iwapo inaamini kuwa kudumisha uwekaji wa sasa wa mtoto unaweza kwa kiasi kikubwa kusababisha jeraha kwa mtoto au kwa wengine.

### Mamlaka ya afisa wa usikilizaji wa kesi

Afisa wa usikilizaji wa kesi anayeafikia masharti yaliyoelezwa katika kichwa kidogo **Afisa wa Usikilizaji wa Kesi Asiyependelea** anapaswa kutekeleza usikilizaji wa mchakato yakinifu na kufanya uamuzi. Afisa wa usikilizaji wa kesi anaweza:

1. Kumrudisha mtoto aliye na ulemavu katika uwekaji ambapo mtoto aliondolewa iwapo afisa wa usikilizaji wa kesi atabaini kuwa uondoaji ulikiuka masharti yaliyoelezwa chini ya mada ya **Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule**, au tabia ya mtoto ilikuwa ni udhihirisho wa ulemavu wa mtoto; **au**
2. Kuamuru ubadilishaji wa uwekaji wa mtoto aliye na ulemavu kwa mazingira mbadala ya elimu ya muda inayofaa kwa siku zisizozidi 45 iwapo afisa wa usikilizaji wa kesi atabaini kuwa kudumisha uwekaji wa sasa wa mtoto unaweza kwa kiasi kikubwa utasababisha jeraha kwa mtoto au kwa wengine.

Taratibu hizi za usikilizaji wa kesi zinaweza kurudiwa, iwapo SAU inaamini kuwa kumrudisha mtoto katika uwekaji halisi kunaweza kwa kiasi kikubwa kusababisha jeraha kwa mtoto au kwa wengine.

Kila wakati mzazi au SAU inawasilisha *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu ili kuomba usikilizaji wa kesi kama huu, usikilizaji wa kesi ni lazima ufanyike ambao unatimiza masharti yaliyoelezwa chini ya kichwa **Maombi ya Usikilizaji wa Mchakato Yakinifu** isipokuwa kama vifuatavyo:

1. Shirika la Elimu la Jimbo inapaswa kupangia usikilizaji wa mchakato yakinifu ulioharakishwa, ambao ni lazima ufanyike ndani ya siku **20** za shule kutoka tarehe ambapo usikilizaji uliombwa na ni lazima usababishe uamuzi ndani ya siku **10** za shule baada ya usikilizaji wa kesi.

2. Isipokuwa iwapo wazazi na shule wakubaliane kwa maandishi kuondoa mkutano, au kukubaliana kutumia upatanishi, mkutano wa usuluhishi ni lazima ufanyike ndani ya siku **saba** za kalenda baada ya kupokea *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu. Usikilizaji unaweza kuendelea isipokuwa iwapo jambo hili limesuluhishwa hadi pande zote mbili ziridhike ndani ya siku **15** za kalenda baada ya kupokea *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu.
3. Jimbo linaweza kuweka masharti tofauti ya usikilizaji wa kesi ulioharakishwa kuliko kama ilivyoweka katika usikilizaji mwingine wa kesi, isipokuwa kwa ratiba za nyakati, masharti haya yanapaswa kufanana na masharti katika hati hii kuhusiana na usikilizaji wa kesi.

Mhusika anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo katika usikilizaji wa mchakato yakinifu katika njia ileile kama ziwezavyo katika maamuzi ya usikilizaji wa mchakato yakinifu (angalia **Rufaa**, hapo juu).

## Uwekaji Wakati wa Rufaa
## 34 CFR §300.533

Wakati ambapo, kama ilivyoelezwa hapo juu, mzazi au SAU iwasilishe *ombi la usikilizaji* wa mchakato yakinifu kuhusiana na mambo ya kinidhamu, mtoto anapaswa (isipokuwa iwapo mzazi na Shirika la Elimu la Jimbo au SAU wakubaliane vinginevyo) kubaki katika mazingira mbadala ya elimu ya muda akisubiri uamuzi wa afisa wa usikilizaji, au hadi kuisha kwa wakati wa kipindi cha uondoaji kama ilivyotolewa kwa na kuelezwa chini ya kichwa **Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule**, yoyote inayotokea kwanza.

## Ulinzi wa Watoto Ambao Bado Hawastahiki Elimu Maalum na Huduma Husika
## 34 CFR §300.534

**Jumla**

Iwapo mtoto hajabainishwa kustahiki elimu maalum na huduma husika na anakiuka kanuni za maadili ya wanafunzi, lakini SAU ilifahamu (kama ilivyobainishwa hapo chini) kabla ya kutokea kwa tabia iliyosababisha hatua ya kinidhamu kuwa mtoto alikuwa ni mtoto aliye na ulemavu, basi mtoto anaweza kusisitiza yoyote ya ulinzi ulioelezwa katika taarifa hii.

Msingi wa ufahamu wa masuala ya kinidhamu

SAU itachukuliwa kuwa ilifahamu mtoto ni mtoto aliye na ulemavu iwapo, kabla ya kutokea kwa tabia iliyosababisha hatua ya kinidhamu:

1. Mzazi wa mtoto alionyesha wasiwasi wake kwa maandishi kwamba mtoto anahitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa wafanyakazi wa usimamizi au utawala wa shirika linalofaa la elimu au mwalimu wa mtoto;
2. Mzazi aliomba tathmini inayohusiana na ustahiki wa elimu maalum na huduma husika chini ya Sehemu ya B ya IDEA; **au**
3. Mwalimu wa mtoto au mfanyakazi mwingine wa SAU alionyesha wasiwasi mahususi kuhusu mtindo wa tabia iliyoonyeshwa na mtoto moja kwa moja kwa msimamizi elimu maalum wa SAU au kwa mfanyakazi mwingine wa usimamizi wa SAU.

Kighairi

SAU haitachukuliwa kuwa na ufahamu kama huo iwapo:

1. Mzazi wa mtoto hajaruhusu tathmini ya mtoto au amekataa huduma za elimu maalum; **au**
2. Mtoto ametathminiwa na kubainishwa kuwa sio mtoto aliye na ulemavu chini ya Sehemu ya B ya IDEA .

Hali zinazotumika iwapo hakuna msingi wa ufahamu

Iwapo kabla ya kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtoto, SAU haina ufahamu kuwa mtoto huyo ni mtoto mwenye ulemavu kama ilivyoelezwa hapo juu chini ya vichwa **Msingi waufahamu wa masuala ya kinidhamu** na **Kighairi**, mtoto anaweza kuchukuliwa hatua za kinidhamu ambazo zinatumika kwa watoto wasio na ulemavu ambao wanajihusisha katika tabia zinazofanana.

Hata hivyo, iwapo ombi litafanywa kutaka tathmini ya mtoto wakati wa kipindi cha wakati ambapo mtoto anachukuliwa hatua za kinidhamu, tathmini ni lazima ifanyike katika namna iliyoharakishwa.

Hadi tathmini ikamilike, mtoto anabakia katika uwekaji wa kielimu unaobainishwa na mamlaka za shule, ambao unaweza kujumuisha usimamishaji na ufukuzwaji bila huduma za kielimu. Iwapo mtoto atabainishwa kuwa mtoto mwenye ulemavu, kwa kuzingatia maelezo kutoka kwa tathmini iliyofanywa na SAU na maelezo yaliyotolewa na wazazi, SAU ni lazima itoe elimu maalum na huduma husika kulingana na Sehemu ya B ya IDEA, ikiwa ni pamoja na masharti ya kinidhamu yaliyoelezwa hapo juu.

## Pendekezo la na hatua ya utekelezaji wa sheria na mamlaka za mahakama
## 34 CFR §300.535

Sehemu ya B ya IDEA haiwezi:

1. Haikatazi shirika kuripoti uhalifu unaofanywa na mtoto aliye na ulemavu kwa mamlaka zinazofaa; **au**
2. Haizuii utekelezaji wa sheria na mamlaka za mahakama za Jimbo kutekeleza majukumu yao kulingana na matumizi ya sheria za Jimbo na Shirikisho kwa hatia zilizofanywa na mtoto aliye na ulemavu.

Usambazaji wa rekodi

Iwapo SAU itaripoti uhalifu uliofanywa na mtoto aliye na ulemavu, SAU:

1. Ni lazima ihakikishe kuwa nakala za elimu maalum ya mtoto na rekodi za kinidhamu zimesambazwa ili kuzingatiwa na mamlaka ambazo mashirika yanaripoti uhalifu; **na**
2. Inaweza kusambaza nakala za elimu maalum na rekodi za kinidhamu za mtoto kwa kiwango tu kinachoruhusiwa na Sheria za Haki za Elimu kwa Familia na Faragha (FERPA).

# Masharti ya Uwekaji wa Upande Mmoja na Wazazi wa Watoto katika Shule Binafsi kwa Gharama ya Umma

## Jumla
## 34 CFR §300.148

Sehemy ya B ya IDEA haihitaji SAU kulipia gharama za elimu, ikiwa ni pamoja na elimu maalum na huduma husika, kwa mtoto wako aliye na ulemavu katika shule au kituo cha kibinafsi iwapo SAU ilitoa elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako na unachagua kumweka mtoto wako katika shule au kituo cha kibinafsi. Hata hivyo, SAU ambapo shule ya kibinafsi ipo ni lazima ijumuishe mtoto wako katika idadi ya watu ambao mahitaji yao yanashughulikiwa chini ya sheria za Sehemu ya B ya IDEA kuhusiana na watoto ambao wamewekwa na wazazi wao katika shule ya kibinafsi chini ya 34 CFR §§300.131 through 300.144.

**Malipo kwa uwekaji wa shule binafsi**

Iwapo mtoto wako hapo awali alipokea elimu maalum na huduma husika chini ya mamlaka ya SAU na uliamua kuchagua kumwandikisha mtoto wako katika shule ya chekechea, shule ya msingi, au shule ya upili ua kibinafsi bila idhini ya au pendekezo la SAU, mahakama au afisa wa usikilizaji wa kesi anaweza kuhitaji shirika kukurejeshea gharama ya uandikishaji iwapo mahakama au afisa wa usikilizaji wa kesi atagundua kuwa shirika haikutoa elimu ya umma inayofaa ya bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako kwa wakati unaofaa kabla ya uandikishaji huu na kuwa uwekaji huu katika shule ya kibinafsi unafaa. Afisa wa usikilizaji wa kesi au mahakama inaweza kuamua kuwa uwekaji wako unaofaa hata iwapo uwekaji hauafikii viwango vya Jimbo ambavyo vinatumika katika elimu inayotolewa na Shirika la Elimu la Jimbi na SAU.

**Kikomo cha malipo**

Gharama ya malipo iliyoelezwa katika aya iliyo hapo juu inaweza kupunguzwa au kukataliwa:

1. Iwapo: (a) Katika mkutano wa hivi majuzi wa mpango wa elimu mahususi (IEP) uliohudhuria kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako kwa shule ya umma, hukuarifu Timu ya IEP kwamba ulikuwa unakataa uwekaji uliopendekezwa na SAU ili kutoa FAPE kwa mtoto wako, ikiwemo kutaja wasiwasi wako na nia yako ya kumwandikisha mtoto wako katika shule binafsi kwa gharama ya umma au (b) Angalau siku 10 za kazi (ikiwemo likizo zinazotokea katika siku ya shule) kabla ya kumwondoa mtoto wako kwenye shule ya umma, hukutoa taarifa ya maandishi kwa SAU kuhusu taarifa hiyo;

**1.** Iwapo, kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako kutoka shule ya umma, SAU ilitoa taarifa ya awali iliyoandikwa kwako, kuhusu nia yake ya kumtathmini mtoto wako (ikiwemo taarifa ya madhumuni ya tathmini iliyofaa), lakini hukuhakikisha kwamba mtoto alikuwepo wakati wa tathmini; **au**

2. Baada ya mahakama kugundua kwamba hatua zako

hazikufaa. Hata hivyo, gharama ya kurejesha fedha:

1. Haipaswi kupunguzwa au kukataliwa kwa sababu ya kutoa taarifa iwapo: (a) Shule ilikuzuia kutoa taarifa; (b) Hukuwa umepokea taarifa ya

wajibu wako wa kutoa taarifa iliyotolewa hapo juu (c) Kuzingatia mahitaji yaliyo hapo juu kunaweza kusababisha kujeruhiwa kwa mtoto wako; **na**

2. Inaweza, kwa uamuzi wa mahakama au afisa wa usikilizaji, kutopunguzwa au kukataliwa kwa sababu ya kushindwa kwa wazazi kutoa taarifa inayohitajika ikiwa: (a) Mzazi hajui kuandika na kusoma au hawezi kuandika kwa Kiingereza (b) Kuzingatia hitaji lililo hapo juu kunaweza kusababisha madhara makubwa ya kihisia kwa mtoto.

## Wazazi mbadala
## 34 CFR § 300.519

**Jumla. (a)**

Kila shirika la umma lazima lihakikishe kwamba haki za mtoto zinalindwa wakati—

(1) Hakuna mzazi (kama ilivyofafanuliwa katika § 300.30) anayeweza kutambuliwa;
(2) Shirika la umma, baada ya jitihada zinazofaa, haliwezi kuwapata wazazi;
(3) Mtoto ni mtegemezi wa Jimbo chini ya sheria za Jimbo hilo; au
(4) Mtoto ni kijana asiye na makazi ambaye hajaandamana na yeyote kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 725(6) cha Sheria ya Usaidizi wa Wasio na Makazi ya McKinney-Vento (42 U.S.C. 11434a(6)).

**Majukumu ya shirika la umma (b)**
Majukumu ya shirika la umma chini ya aya ya (a) ya kitengo hiki yanajumuisha uteuzi wa mtu kuwa mzazi mbadala kwa wazazi. Hii lazima ijumuishe mbinu—

(1) Ya kuamua iwapo mtoto anahitaji mzazi mbadala; na
(2) Ya kumpa mtoto mzazi mbadala.

**Wategemezi wa Jimbo. (c)**
Katika kisa cha mtoto ambaye ni mtegemezi wa Jimbo, mzazi mbadala anaweza kuteuliwa vinginevyo na jaji anayesimamia kesi ya mtoto huyo, mradi tu mzazi huyo mbadala anakidhi matakwa katika aya za (d)(2)(i) na (e) za kitengo hiki.

**Vigezo vya uteuzi wa wazazi mbadala (d)**

(1) Shirika la umma linaweza kuchagua mzazi mbadala kwa njia yoyote inayoruhusiwa chini ya sheria ya Jimbo.

(2) Mashirika ya umma lazima yahakikishe kwamba mtu aliyeteuliwa kama mzazi mbadala—

(i) Si mfanyakazi wa SEA, LEA, mtoa huduma wa EIS au shirika jingine lolote linalotoa huduma za uingiliaji wa mapema, utunzaji au huduma nyingine kwa mtoto au mwanafamilia kwa mtoto;
(ii) Hana maslahi binafsi au ya kitaalamu yanayokinzana na maslahi ya mtoto ambaye mzazi mbadala anawakilisha; na
(iii) Ana ujuzi na stadi zinazohakikisha uwakilishaji wa kutosha wa mtoto.

**Mahitaji yasiyo ya mfanyakazi; fidia (e)**
Mtu aliyehitimu vinginevyo kuwa mzazi mbadala chini ya aya ya (d) ya kifungu hiki si

mfanyakazi wa shirika kwa sababu yeye analipwa na shirika hilo kuhudumu kama mzazi mbadala.

**Kijana asiye na makazi asiyeandamana na yeyote (f)**

Katika kisa cha mtoto ambaye ni kijana asiye na makazi asiyeandamana na yeyote, wafanyakazi wanaofaa wa makazi ya dharura, makazi ya mpito, mipango ya kuishi kwa kujitegemea na mipango ya ufikiaji ya mitaani wanaweza kuteuliwa kama wazazi mbadala bila kuzingatia aya ya (d)(2)(i) ya kitengo hiki, hadi mzazi mbadala ateuliwe anayetimiza mahitaji yote ya aya ya (d) ya kitengo hiki.

**Majukumu ya mzazi mbadala (g)**
Mzazi mbadala anaweza kumwakilisha mtoto katika masuala yote yanayohusiana na—
(1) Utambulisho, tathmini na uwekaji wa kielimu wa mtoto; na
(2) Utoaji wa FAPE kwa mtoto.

**Jukumu la SEA (h)**
Ni lazima SEA ifanye jitihada zinazofaa ili kuhakikisha uteuzi wa mzazi mbadala kwa muda usiozidi siku 30 baada ya shirika la umma kuamua kwamba mtoto anahitaji mzazi mbadala.

## Uhamisho wa haki za mzazi anapofika umri wa kuwa mtu mzima. 34 CFR § 300.520

**Jumla (a)**
Jimbo linaweza kutoa kwamba, wakati mtoto mwenye ulemavu anafika umri wa kuwa mtu mzima*(umri wa miaka 18 huko Maine)* hiyo inatumika kwa watoto wote (isipokuwa mtoto mwenye ulemavu aliyebainishwa kuwa hafai chini ya sheria ya Jimbo)—
(1)(i) Shirika la umma lazima litoe taarifa yoyote inayohitajika katika sehemu hii kwa mtoto na wazazi; na
(ii) Haki zote zilizotolewa kwa wazazi chini ya Sehemu ya B ya uhamisho wa Sheria kwa mtoto;
(2) Haki zote zilizotolewa kwa wazazi chini ya Sehemu ya B ya uhamisho wa Sheria kwa watoto ambao wamefungwa katika jela ya watu wazima au watoto, kituo cha urekebishaji cha Jimbo au eneo husika; na
(3) Wakati wowote Jimbo linapotoa uhamishaji wa haki chini ya sehemu hii kwa mujibu wa aya ya (a)(1) au (a)(2) ya kifungu hiki, shirika lazima liarifu mtoto na wazazi kuhusu uhamishaji wa haki.

**Sheria maalum (b)**
Jimbo lazima liweke taratibu za kuteua mzazi wa mtoto mwenye ulemavu au ikiwa mzazi hapatikani, mtu mwingine anayefaa, kuwakilisha maslahi ya kielimu ya mtoto katika kipindi kizima cha ustahiki wa mtoto chini ya Sehemu ya B ya Sheria ikiwa, chini ya sheria ya Jimbo, mtoto ambaye amefikia umri wa kuwa mtu mzima, lakini hajabainishwa kuwa hafai, anaweza kuamuliwa kutokuwa na uwezo wa kutoa ridhaa kuhusiana na mpango wa elimu wa mtoto.